MACHI MMXXV - TOLEO LA XLI

# NGURUMO

*ya Mwandishi*



DR. PEGGY DITHAPELO
LUBINDA

**RIWAYA:**

MSALITI '02' uk 12-13
NAJUTIA KUWA NAWE '01' uk 14-15
HAPPY NEW YEAR '3' uk 26-27
SHEMEJI USIZIME TAA '5' uk 28-29

HISTORIA YA MAISHA YAKO YAWEZA KULETA

# MABADILIKO

KWA WENGINE

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— HISTORIA YA MAISHA YAKO… —Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Asha Siraj —Uk 03

**New In Town:** Saikolojia ya Mahusiano na Ndoa — 04

**PITIO LA VITABU**— NGUZO MAMA—Uk 06

**MAKALA** — **SAIKOLOJIA**: —Uk 06 na 07

**MAKALA:** Umuhimu wa Fasihi kwa Mwanadamu…-uk 08

**MIAMBA WA AFRIKA:** PATRICE LUMUMBA ‘5’— Uk 10

**Sako kwa Bako–** Jalyna Malombe —Uk 11

**RIWAYA:**— MSALITI ‘2’—Uk 12 na 13

**RIWAYA—** Najutia Kuwa Na Wewe-Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Alibaba na Wezi 40 ‘17’- Uk 16

**HABARI:** TUZO ZA TUCHAWA – Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** HISTORIA YA VITABU ‘Kitabu cha Wafu’—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA:** UJANAJIKE —Uk 19

**MATANGAZO: -** Uk 20

**MALENGA WA KILEO:** Nawapongeza washindi — Uk 21

**HABARI PICHA: -** TUZO ZA TUCHAWA-Uk 22

**KUTOKA MAKTABA:** Maisha ni Mapambano ‘8’-Uk 23

**ELIMU JAMII:** — Mabadiliko ya Tabia Nchi —Uk 24

**HADITHI:** — Happy New Year ‘4’ Uk. 26 na SHEMEJI USIZIME TAA…! ‘5’ —27

## TAHARIRI:
## HISTORIA YA MAISHA YAKO YAWEZA LETA MABADILIKO KWA WENGINE

Asalaam,

Ni matumaini yangu kuwa mu wazima kabisa. Ni wakati mwingine tena tunakutana katika toleo hili la 41 kwa kusema kuwa ‘Historia ya maisha yako yaweza leta mabadiliko kwa wengine’, je unaamini katika hili?

Kwa upande wangu mimi, jibu ni ‘ndiyo’. Yakupasa ujue kuwa historia ya kila mtu duniani ina funzo kwa mwingine. Hata historia yako wewe unayesoma hapa sasa, endapo utaisimulia kwa mwingine lazima itamuachia funzo fulani na kama mtu huyo akitaka kulifanyia kazi funzo hilo basi bila shaka atapata mabadiliko.

Umeshawahi kufikiri kuandika historia yako ya maisha? Iwe mbaya au nzuri, vyovyote vile. Kama ‘ndiyo’ basi fanya haraka kuanika kwani kuna watu wanasubiri funzo kutoka kwako. Kama ‘hapana’ basi kaa chini ufikiri kwa mara ya pili juu ya hilo.

Ukipita kwenye maduka ya vitabu utakutana na vitabu vingi vya historia za watu mbalimbali, wanasiasa, wafanyabishara, wanamichezo, madaktari, waalimu, wanafasihi nk. Na ukisoma ndani yake utakutana na mafunzo mengi sana ambayo kwayo waweza kupata mabadiliko kama ukiyafanyia kazi.

Basi, weka wazi historia yako, simulia watu, andika kitabuni ili wengine wakusome, wakujue, wakuige au wajifunze kutoka kwako. Acha uchoyo!

Nakutakieni sikukuu ya Pasaka iliyo njema kwenu nyote!

Amata Ric Richard Mwambe
Jamvi la Simulizi—Ngurumo ya Mwandishi
5/4/2025
Mawelewele—Iringa

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

## MWANDISHI WETU:

## ASHA SIRAJ

JAMVI la SIMULIZI

**Katika safu yetu pendwa siku ya leo, tunamkaribisha mwanadada mrembo Asha Siraj. Kwa wapenzi wa Facebook jina hili si geni kwani huko anaunguruma haswa!**

**Bai hebu tumsome, tumjue, tutafute kazi zake, tuburudike. Asha, karibu...**



ASHA SIRAJ

Kiufupi story yangu... Me' nimezaliwa Bukoba Mjini, kabila langu ni muhaya. Ila kwa sasa naishi Mwanza japo huwa ni mtu wa kusafiri sana.

Elimu yangu me' ni ya chini sana, nimeishia *form Three* baada tu ya wazazi wangu kutengana, hivo nilishindwa kupata mtu wa kuniendeleza kielimu, ila tokea nipo shule nilikuwa napenda sana kusoma *story*. Hali hiyo iliniathiri. Nakumbuka kulikuwa kuna kipindi ikifika saa kumi na mbili baba angu alikuwa anapenda kuwasha redio kwa ajili ya kusikiliza simulizi. Basi me' nilikuwa nikiacha kazi zangu na kukimbilia karibu na redio kwa ajili ya kusikiliza hadithi.

Kuna mda nilivyokuwa nikitoka shule basi naacha kufanya kazi zangu naanza kuandika hadithi. Maisha yangu yaliendelea kuwa hivyo.

Nilianza kuandika hadithi huku nikiwa nawatumia watu WhatsApp baada ya kumiliki simu kubwa na nyingine nilifanya kuzipost FB. Niliendelea kufanya hivyo. Nilikuja kupata bahati siku moja, nakumbuka siku hiyo nilipigiwa simu na binti mmoja wengi wanamjua anatumia jina la SUMAIYA MWENDO katika uandishi wake. Ndiye mtu aliyeweza kuniinua juu baada ya kuniambia hadithi hizi pia zinauzwa na akadai naweza kupata ridhiki yoyote ile. Aliniunganisha na baadhi ya waandishi na kweli waliitikia wito nilianza kufanya nao kazi na tukaunda *group* moja linaitwa SIMULIZI HOUSE. Basi walianza kuniunga baadhi ya ma*group* mpaka sasa bado naendelea na uandishi. Niseme namshukuru Mungu mpaka sasa nilipofikia.

Kiufupi mpaka sasa sijaandika vitabu me' ni mtu wa kuandika hadithi nakutuma kwenye ma*group*, hivo sijabatika kuandika kitabu na nina ndoto sana yakuwa muandishi mashuhuri hapa nchini hasa pale nitakapopata mtu wa kunishika mkono.

Kwenye uandishi kuna changamoto nyingi sana. Changamoto ambayo mpaka sasa inaniumiza kichwa ni pale mtu unapokuwa unatumia mda mwingi kuiandaa kazi yako alafu baada ya kuanza kuiuza, unakuta tayari imeshaibwa, na watu wengi nao wapo wanaiuza. Hii kitu huwa inaniuma sana kiufupi.

Sina uzoefu sana kwenye soko la vitabu. Kiufupi sina neno kwasababu bado sijapata changamoto hiyo

Namhusudu sana mwandishi AMANI KIGOYA. Ni mwandishi ambaye huwa namkubali sana hapa nchini

Kiufupi kazi zangu huwa natuma kwenye ma*group* ya WhatsApp nina baadhi ya ma*group* ya waandishi tofauti tofauti huwa na*post* huko n.k na FACEBOOK pia napost. Kwa wasomaji, niseme tu nawapenda sana waendelee kufuatilia hadithi zetu, kuna vitu vingi vya kujifunza kupitia hadithi zetu japo watu huwa wanazidharau hadithi ila kiufupi kuna mambo mengi ya kujifunza ndani mwake haswa Katika jamii yetu hii inayotuzunguka, hadithi nikama unavyoona *movies*.

*Asha Siraj ni mwandishi chipukiz wa kike. Ni mmoja kati ya wasichana wenye uthubutu katika sanaa hii ya uandishi na fasihi. Katika toleo hili tutaanza kusoma moja ya simulizi zake yenye anwani 'Najutia Kuwa Nawe'.*

*Kama utapenda kumshika mkono kama mfadhili wa kuchapa vitabu vyake, basi mawasilino yake ni haya hapa.*

*Whatsapp 0789044345*

# NEW IN TOWN :
## SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA

KATIKA maisha ya mwanadamu lazima hatua ya kupenda na kupendwa aipitie. Maisha bila mapenzi hayajakamilika bado. Ni lazima mwanadamu aipitie hatua hii.

Kitabu SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA ni jibu la matatizo mengi yahusuyo Nyanja ya mapenzi na hatua zake. Yapo mambo mbalimbali yatatizayo mahusiano na ndoa, kitabu hiki ni suluhisho la mambo hayo.

Nifanye nini ili mpenzi wangu anipende? Ni swali ambalo watu wengi limewatatiza, hasa pale waonapo mapenzi yamepungua. Wengi wamepita njia za mkato katika kutatua matatizo yao. Kitabu hiki kiwe jibu la swali hilo na maswali mengine.

NEEMA ELIAS MGAO ni mwandishi wa makala na vitabu vya saikolojia, pia ni mshauri wa masuala yahusuyo mahusiano, ndoa, malezi ya watoto na vijana na masuala yote ya maisha kwa ujumla.  Msuluhishi na mpatanishi anayeamini katika kupatanisha watu.

Amefanya kazi mbalimbali za kufundisha na kuelimisha kuhusiana na  masuala ya  saikolojia kwa makundi au kwa mtu binafsikatika sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Neema anaamini katika falsafa ya mazungumzo na maelewano ili kuleta amani mahali popote pale katika maisha.

Kupata kitabu hiki wasiliana na mwandishi kwa namba 0763013206.
Pia utakipata katika maduka ya vitabu,

- Dar es salaam Kona ya Riwaya Kinondoni au piga simu **0655428085**
- Posta Mpya kwa Joji au piga simu **0713454152**
- Dodoma wasiliana na mtunzi kwa namba **0763013206**
- **Popote mkoani kinatumwa na kitakufikia salama.**





MALKIA wa Kiha, mwanamama machachari kutoka Morogoro, muelimishaji na mshauri, mwandishi wa kitabu cha Tunu Sita za Malezi anakuja na kitabu kipya kabisa chenye anwani MWANDAE MTOTO WA KIUME KUWA MWANAUME.

Kwa mujibu wa taarifa yake ni kuwa kitabu hiki kitapatikana  kuanzia tarehe 26/4/2025.

Ni kitabu kinachofaa sana kwa wazazi kujifunza namna bora ya kumlea mtoto wa kiume, kumfanya ajitambue na ajiandae kwa majukumu yake ya baadae. Pia amesema kuwa ofa bado haijaisha, wahi sasa wasiliana naye kwa simu ulipie punguzo.

Ngurumo ya Mwandishi tunampongeza sana kwa kitabu hiki cha malezi na katika matoleo yajayo basi tutakizungumzia zaidi.

Wahi sasa, changamkia ofa kwa kupiga namba hizo hapo mkwenye tangazo lenyewe.



# NGUZO MAMA—2

**PITIO LA VITABU**

**KITABU – NGUZO MAMA**

**MWANDISHI – PENINA MHANDO**

**WACHAPISHAJI – DUP**

**MWAKA – 1982**

**MHAKIKI: MWALIMU MAKOBA**

Inaendelea...

iii. Picha na taswira

- Nguzo mama

Hii ni lugha ya picha ambapo neno nguzo mama linaashiria ukombozi wa mwanamke, nguzo mama ni mambo yote mazuri ambayo anayahitaji mwanamke ili akombolewe, mwanamke anajitahidi kupambana kuiinua nguzo mama lakini anashindwa.

**4. Wahusika**

i. Bi Moja

- Mke wa Shabani

- Hana msimamo katika kuisiamisha nguzo mama

ii. Bi Pili

- Mke wa Sudi

- Ananyanyaswa na mume wake

iii. Bi Tatu

- Anabembeleza mume wake kwa kuogopa kuachwa

- Ni mpenda starehe

iv. Bi Nne

- Hapendi maendeleo ya watu wengine

v. Bi Tano

- Anahasira sana

- Ni mke wa Maganga

vi. Bi Sita

- Anatembea na waume za watu

vii. Bi Saba

- Shemeji zake walimnyang'anya mali mara baada ya kufiwa na mumewe

viii. Bi Nane

- Alipenda kuelimisha wenzake katika shughuli za maendeleo

ix. Chizi

- Ni mfichua maovu yaliyoko katika jamii

x. Mwenyekiti

- Ni kiongozi mbaya tena asiye na elimu

**Mandhari**

Msanii anatumia madhari ya kubuni ya mji wa Patata. Tamthiliya hii imetendeka katika mandhari ya,

- Vilabuni


- Uwanjani

- Mtaani

**Kufaulu kwa mwandishi**

Amefaulu kuonesha matatizo yanayowapata wanawake. Matatizo hayo ni kama, manyanyaso, umasikini, ukosefu wa elimu na uongozi mbaya.

Pia mwandishi ametumia lugha rahisi inayoeleweka kwa awasomaji wengi




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

**Kutofaulu kwa mwandishi**

Hitimisho la kushindwa kuiinua nguzo mama kwa wanawake linakatisha tamaa na kupeleka ujumbe kuwa, matatizo ya wanawake hayawezi kuondoka.

***MWISHO***

**PICHA YA JALADA**

**DR. PEGGY DITHAPELO LUBINDA**

**Mshindi wa THE AFRICAN WRITING TRIBE**

**'AUTHOR OF THE YEAR'**



**SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA.**

Uhali gani mpenzi msomaji wa jarida hili la NGURUMO YA MWANDISHI, katika toleo hili nitazungumzia kidogo kitabu hiki cha SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA.

Ni baada ya kutazama mwenendo wa mahusiano au ndoa za siku hizi kwa muda mrefu, kutokana na kazi niifanyayo ya kushauri maswala mbalimbai yahusuyo mahusiano,mapenzi,ndoa,malezi ya watoto na vijana na maisha kwa ujumla,kazi niliyoifanya na nayoendelea kuifanya kwa muda wote,kwa Zaidi ya miaka 15 sasa. Baada ya kuitazama hali halisi ya mahusiano na ndoa za siku hizi, ndipo nikaona ni wakati sahihi sasa wa kuandika na kutoa kitabu hiki cha SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA.

Kitabu hiki ni utafiti nilioufanya kwa miaka zaidi ya 7 sasa katika nyanja hii ya mapenzi, mahusiano,na ndoa. Maandalizi ya kitabu hiki yamekamilishwa kiukamilifu na kinakidhi na kufaa kwa matumizi ya walio kwenye mahusiano, walio kwenye mapenzi na walio kwenye ndoa pia. Ndani ya kitabu hiki nilibahatika kufanya mahojiano yenye lengo la kukusanya elimu na maoni juu ya mapenzi/mahusiano. Shukrani za kipekee ziwaendee MH. MICHAEL SIMON diwani wa kata ya KIWIRA, MBEYA –TANZANIA, mwandishi SAIDY MBAGATI [Mwandishi Mbagati], na MH. JOHN KUMBULWA ambae yeye ni jaji katika mahakama ya mkoani MOROGORO – TANZANIA. Mwandishi JONATHAN NGUA ametubarikia sura nzima iliyosheheni uvumbuzi wa matatizo katika mahusiano na ndoa kwa ujumla  na utatuzi wake.

SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA ni kitabu kilichojikita katika kuainisha na kuonyesha namna ya kushughulikia changamoto mbalimbali. Mwanadamu ili akamilike,ni9 lazima apitie hatua ya kupenda na kupendwa. Sasa katika safari ya kukamilisha hatua hiyo ya mapenzi,yapo mambo mengi binadamu anaweza kuyapitia. Zipo changamoto nyingi ambazo zisipotatuliwa kwa uweredi hupelekea wapenzi husika kufanyiana mambo ya ajabu kama kudhuriana na pengine hata kuua au kujiua.


Kitabu hiki kiko na mambo mengi mazuri ambayo utayafanya ili kutatua migogoro mbalimbali katika maqisha ya mapenzi,mahusiano,na ndoa yako.

PATA COPY YAKO KUPITIA NAMBA +255 763 013 206 au nifuate kwenye mtandao wa FACEBOOK ili kujua sehemu zingine ambazo utapata kitabu hiki. Karibu.

**Madame Neema Mgao,**

**The Magic Author,**

**Queen of psychology.**



# ROSA MISTIKA

## ROSA MISTIKA YAJA KWA KIINGEREZA

KWA wapenzi wa fasihi hapa Tanzania, hawatakuwa wageni na jina la kitabu hiki "ROSA MISTIKA". Hii ni moja ya kazi bora sana kutoka kwenye mkono wa EuEuphrase Kezilahabi.

Wengi wetu tumekisoma na hakuna kati yetu atakayesema kuwa kitabu kile kibaya, hakivutii. Badala yake kila mmoja anakisifia kitabu hicho.

Katika pitapita zetu juma hili tumekutana na hii barua iliyobeba ujumbe mzito na wa kuvutia ya kuwa, Riwaya "Rosa Mistika" imetasfiriwa kwenye lugha ya Kiingereza na iko mbioni kuchapwa kitabu. Ni nani, na anasemaje? Hii hapa!

*Zingatia, hii ni tafsiri isiyo rasmi ya barua iliyotufikia…*

Mpendwa Profesa Senkoro,

Natumai ujumbe huu umekufikia ukiwa mzima wa afya! Jina langu ni Abigail Storch, mimi ni mhariri katika idara ya uchapaji ya Chuo Kikuu cha Yale, ambapo ninasimamia mfululizo wetu wa *Margellos World Republic of Letters* unaohusu fasihi ya tafsiri kutoka lugha mbalimbali.

Ninayo furaha kukushirikisha habari kwamba mnamo Juni 17, idara ya ya uchapaji ya Chuo Kikuu cha Yale itaichapa 'Rosa Mistika ya Euphrase Kezilahabi, tamthilia ya Kiswahili iliyozua utata kutoka kwa mmoja wa waandishi wanaoheshimika sana nchini Tanzania, iliyopigwa marufuku wakati wa kuchapishwa kwake kwa mara ya kwanza, na sasa imetafsiriwa kwa Kiingereza na Jay Boss Rubin.

Rosa, msichana wa umri wa ujana, anaishi na wazazi wake pamoja na dada zake wanne wadogo katika kijiji kilichoko Kisiwa cha Ukerewe ndani ya Ziwa Victoria, ambako huhudhuria shule ya kijiji na kusaidia kazi za shamba la familia. Maisha yangekuwa ya utulivu kiasi kama si kwa sababu ya baba yake Rosa, ambaye hujinywea pombe kupita kiasi na kuwatukana matusi na kumtendea ukatili mkewe pamoja na binti zake. Akiwa na faraja kwa kukubaliwa kujiunga na shule ya bweni bara, Rosa anatambua kuwa hana maandalizi ya kutosha kwa maisha nje ya kijiji chao. Kadri anavyozoea hila za wanaume na kupata matunzo toka kwao, anaanza kuelewa kuwa jinsia yake inaweza kuwa silaha. Lakini uelewa huu, uliozaliwa kutokana na hitaji la kuishi katika dunia ya viwango viwili, unakuja kwa gharama.

Rosa Mistika ni simulizi ya kishujaa kuhusu uanamke, upendo wa mama, uwezo binafsi, na mamlaka—na ni riwaya ya kwanza kabisa ya Kiswahili kushughulikia masuala ya unyanyasaji wa nyumbani, kulazimishwa kingono, na utoaji mimba. Kupitia hadithi ya msichana huyu na jamii yake, riwaya hii inauliza swali la kudumu: Kwa kiwango gani tunawajibika kwa maamuzi tunayofanya, na kwa kiwango gani tunaathiriwa na nguvu zilizo nje ya uwezo wetu?

Kitabu hiki tayari kimepokelewa kwa sifa nyingi; nimejumuisha baadhi ya maoni hapa chini:

"Riwaya muhimu sana." — Abdulrazak Gurnah, mshindi wa Tuzo ya Nobel ya Fasihi 2021.

"Imetafsiriwa kwa uangalifu na uzuri mkubwa, Rosa Mistika ni tafakari ya kina juu ya jinsi tunavyopata uhuru binafsi, kama wanawake na wanaume waliokuzwa katika mfumo dume, na katika jamii zinazovaa mabaki ya ukoloni—na kisha tunapopewa uhuru, tunaufanyia nini." — Mũkoma wa Ngũgĩ, mwandishi wa *The Rise of the African Novel: Politics of Identity, Language and Ownership.*

"Mwanzo ilipigwa marufuku, riwaya nzuri ya Euphrase Kezilahabi Rosa Mistika sasa ni lazima isomwe. Rosa ni jasiri, wala si mjinga wala mhanga. Anawajua wanaume katika simulizi hii ya kushangaza lakini ya kweli kabisa, lakini mambo hayaendi vizuri. Lazima apambane vikali kuepuka vizingiti vya baba yake, viwango viwili, tamaa, na uanamama. Rosa Mistika italeta maisha ya maadili ya Kitanzania kwa wasomaji wapya duniani kote, na itakuwa riwaya ya kipekee kwa wanawake duniani kote." — Teresa Svoboda, mshindi wa Tuzo ya Graywolf ya Uandishi wa Uhalisia.

"Katika tafsiri bora ya Jay Boss Rubin, nilihisi kama ninasoma tena Rosa Mistika kwa Kiswahili, lakini pia kama ninakisoma kwa mara ya kwanza. Kuna lugha mbili hapa, si tu moja ikichukua nafasi ya nyingine. Kazi ya ajabu ya tafsiri." — Idza Luhumyo, mshindi wa Tuzo ya AKO Caine 2022 kwa Uandishi wa Kiafrika.

Tafadhali jisikie huru kushirikisha taarifa hizi na wenzako, na pia na maktaba ya chuo au taasisi unayofanyia kazi, pamoja na mtu mwingine yeyote unadhani anaweza kuwa na shauku ya kusoma kitabu hiki. Kama wewe ni profesa, tutathamini pia ikiwa utaweza kufikiria kukifundisha katika kozi zako. Kama wewe ni mwandishi, tungependa pia kupokea mapendekezo ya ukaguzi kutoka kwako! Nimeambatisha nakala ya e-galley kwa ajili ya kukuvutia. Tafadhali nijulishe ikiwa ungependa nakala ya kuchapishwa kwa ajili ya kufanya ukaguzi au mahojiano.

Natumai kitabu hiki kitakugusa, kama kilivyowagusa wengi wetu hapa Idaya ya uchapaji ya Chuo Kikuu cha Yale .

Kwa heri ya moyo,
Abigail Storch | Mhariri Msaidizi
Yale University Press

# Umuhimu wa Fasihi Katika Maisha ya Mwanadamu

**Na Mwandishi wetu**

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kwa namna ya kipekee ili kueleza hisia, mawazo, maadili, na masuala mbalimbali ya kijamii. Katika maisha ya mwanadamu, fasihi ina nafasi kubwa na ya kipekee ambayo haiwezi kupuuzwa. Hapa chini ni baadhi ya sababu zinazodhihirisha umuhimu wa fasihi katika maisha ya binadamu:

**1. Kuhifadhi na Kukuza Utamaduni**

Fasihi ni hazina ya historia na utamaduni wa jamii. Kupitia hadithi, mashairi, methali na semi, jamii huweza kuendeleza mila na desturi zao. Fasihi hurithisha maadili na maarifa kutoka kizazi kimoja hadi kingine, hivyo kuimarisha utambulisho wa jamii.

2. **Kuelimisha Jamii**

Fasihi ina uwezo wa kufundisha kupitia simulizi. Kupitia wahusika na matukio ya kifasihi, wasomaji hujifunza kuhusu tabia nzuri na mbaya, athari za maamuzi, na namna ya kushughulikia changamoto mbalimbali za maisha. Fasihi huleta maarifa kwa njia nyepesi na ya kuvutia.

**3. Kuburudisha**

Moja ya kazi kuu za fasihi ni kuburudisha. Hadithi za kusisimua, mashairi yenye vina na mizani, na tamthilia za kuigiza huwaondolea watu mawazo na kuwapa furaha. Fasihi huleta faraja hasa katika nyakati ngumu za maisha.

**4. Kuchochea Fikra na Kuibua Mijadala**

Fasihi huchochea tafakuri juu ya masuala nyeti ya kijamii kama vile rushwa, ukabila, ukandamizaji wa haki, na uongozi mbovu. Kupitia kazi za kifasihi, waandishi huibua mijadala inayochangia kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

**5. Kukuza Lugha**

Fasihi huimarisha matumizi ya lugha. Kupitia kusoma na kuandika kazi za kifasihi, watu huongeza msamiati wao, ufasaha wa lugha, na uwezo wa kujieleza kwa ufasaha zaidi. Pia, fasihi husaidia katika kuhifadhi lugha za asili zinazotishiwa na kuangamia.

**6. Kujenga Uelewa wa Kibinadamu**

Fasihi hutufanya tuwaelewe watu wengine kwa undani zaidi. Wahusika wa kifasihi mara nyingi huakisi maisha halisi ya binadamu – mapenzi yao, huzuni, matumaini, na maumivu. Hii huongeza huruma, uelewa na mshikamano miongoni mwa watu.

**7. Kutoa Nafasi ya Kujieleza**

Kwa waandishi na wasanii wa fasihi, kazi zao ni jukwaa la kujieleza. Hutoa fursa ya kueleza hisia, ndoto, na mitazamo yao juu ya maisha, hivyo kusaidia pia katika uponyaji wa kihisia na kisaikolojia.

**Fasihi ya Kiafrika**

Fasihi ya Kiafrika ni mkusanyiko wa kazi za kifasihi zinazotokana na maisha, tamaduni, historia, na fikra za watu wa Afrika. Inaweza kuandikwa kwa lugha za Kiafrika kama Kiswahili, Kizulu, Kiyoruba

.

Kwa ujumla, fasihi ya Kiafrika imegawanyika katika makundi makuu mawili:

**1. Fasihi Simulizi**

Hii ni fasihi inayopitishwa kwa maneno ya mdomo kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Mifano: hadithi za kusisimua *(ngano),* methali, nahau, vitendawili, nyimbo za jadi, na mashairi ya asili.

Fasihi hii imekuwa na nafasi kubwa katika kuhifadhi historia, maadili, na maarifa ya jamii mbalimbali barani Afrika.

**2. Fasihi Andishi**

Hii ni fasihi iliyorekodiwa kwa maandishi.

Ilianza kushamiri hasa wakati wa ukoloni na baada ya uhuru.

Waandishi maarufu katika uga huu hapa Afrika ni:

Chinua Achebe (Nigeria) – *Things Fall Apart*

Ngũgĩ wa Thiong'o (Kenya) – *A Grain of Wheat*

Shaaban Robert (Tanzania) – *Kusadikika*

Wole Soyinka (Nigeria) – mshindi wa Tuzo ya Nobel katika Fasihi

Nuruddin Farah (Somalia)

**Maudhui Makuu ya Fasihi ya Kiafrika:**

- Ukoloni na athari zake
- Uhuru na ujenzi wa taifa
- Uongozi na siasa
- Mapambano ya kijamii na kiuchumi
- Utambulisho wa Kiafrika
- Mila, desturi na mabadiliko ya kijamii

- Jinsia na nafasi ya mwanamke katika jamii

Fasihi ya Kiafrika ina nafasi muhimu si tu kwa burudani, bali pia kwa elimu, uhamasishaji, na uhifadhi wa utambulisho wa Mwafrika.

**Hitimisho**
Fasihi ni kioo cha jamii na chombo cha mabadiliko. Kwa kutambua nafasi yake, jamii inaweza kujiendeleza kiutamaduni, kielimu, na hata kiroho. Kuikuza na kuiheshimu fasihi ni kuwekeza katika maendeleo ya mwanadamu kwa ujumla.

---

**TANGAZO**




## Tamasha la Fasihi ya Kiswahili kufanyika Mei 2025

Na Mwandishi wetu.

TAMASHA la Fasihi ya Kiswahili msimu wa tatu 2025 ambalo huandaliwa na Taasisi ya Mfuko wa Fasihi Tanzania (TAFF), linatarajiwa kufanyika mwezi Mei mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Afisa Habari wa TAFF, Bwana Stallone Joyfully, Tamasha hilo la Fasihi ya Kiswahili linatarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam nchini Tanzania katika eneo litakalotangazwa baadae mwezi huu.

"Baada ya kufanya matamasha ya fasihi kwa miaka miwili mfululizo nje ya Dar es Salaam, sasa ni zamu ya Dar es Salaam," alisema Joyfully na kuongeza kwamba ujumbe wa mwaka huu wa Tamasha la Fasihi ya Kiswahili ni RUDISHA KITABU NYUMBANI.

Joyfully alisema kama ilivyokuwa katika matamasha yaliyopita, Tamasha la msimu wa tatu pia litakuwa na mambo kadhaa kama utoaji wa tuzo na zawadi kwa washindi wa mashindano ya utunzi wa hadithi fupi yaliyofanyika septemba mwaka jana, tuzo kwa wanafasihi waliofanya makubwa kwa fasihi pamoja na mijadala ya kuendeleza fasihi ya Kiswahili nchini.

"Tamasha pia litazindua vitabu kadhaa vya fasihi ya Kiswahili pamoja na kuwaleta pamoja wanafasihi kutoka nchi pande mbalimbali za Tanzania ikiwemo Afrika Mashariki." Alisema Joyfully na kuongeza kwamba Tayari nchi za Kenya na Uganda zimethithibitisha kushiriki na miongoni mwa washindi 11 walioiongia katika orodha fupi ya mashindano ya TAFF wawili wanatokea nchini Kenya.

**KATIKA safu yetu ya MIAMBA WA AFRIKA, leo tunakuletea Patrice Lumumba. Huyu alikuwa Waziri Mkuu wa nchi ya Congo DRC. Ni mmoja kati ya waafrika wachache waliokataa kuwa vibaraka wa wakoloni, alipambana kuikomboa Kongo, lakini nini kilimkuta? Tuendelee...**



## Juhudi za Kurudisha Udhibiti

"Serikali imetangaza hali ya hatari katika nchi nzima... Wale wanaochanganya njama za kihaini na uhuru, vizuizi na upinzani wa kidemokrasia, au maslahi yao binafsi na yale ya taifa, hivi karibuni watahukumiwa na wananchi. Wale wanaolipwa leo na maadui wa uhuru kwa ajili ya kudumisha harakati za uasi kote nchini na hivyo kuvuruga amani ya kijamii wataadhibiwa kwa nguvu kubwa kabisa…" Hii ilikuwa kauli ya Lumumba kwa waandishi wa habari, 10 Agosti 1960.

Mnamo tarehe 9 Agosti, Lumumba alitangaza hali ya hatari kote nchini Kongo. Baadaye alitoa amri kadhaa kwa lengo la kurejesha mamlaka yake katika medani ya kisiasa. Amri ya kwanza ilikataza kuundwa kwa vyama au mashirika yoyote bila kibali cha serikali. Amri ya pili ilieleza kuwa serikali ina haki ya kupiga marufuku machapisho yoyote yanayoweza kuichafua serikali au kuharibu heshima yake. Tarehe 11 Agosti, gazeti la *Courrier d'Afrique* lilichapisha tahariri iliyosema kuwa Wakongo hawataki kuangukia "aina ya pili ya utumwa." Mhariri alikamatwa mara moja na baada ya siku nne gazeti hilo lilisitishwa kuchapishwa. Muda mfupi baadaye, serikali ilifunga huduma za habari za Belga na Agence France-Presse.

Lumumba alitangaza utaifishaji wa ofisi za Belga zilizokuwa nchini, na kuanzisha *Agence Congolaise de Presse* kama njia ya kuondoa kile alichokiona kama kituo cha habari chenye upendeleo, pamoja na kujenga chombo cha kueneza sera za serikali kwa urahisi zaidi kwa wananchi. Amri nyingine ilielekeza kuwa idhini ya serikali ilihitajika angalau siku sita kabla ya mikutano ya hadhara kufanyika. Mnamo 16 Agosti, Lumumba alitangaza kuanzishwa kwa *régime militaire spécial* kwa kipindi cha miezi sita.

Katika mwezi wote wa Agosti, Lumumba alianza kujitenga na baraza lake lote la mawaziri na badala yake akaanza kushauriana zaidi na maafisa aliowaamini kama Maurice Mpolo, Joseph Mbuyi, Kashamura, Gizenga, na Antoine Kiwewa. Ofisi ya Lumumba ilikuwa imevurugika sana, na wafanyakazi wachache tu waliokuwa wakifanya kazi. Mkuu wa wafanyakazi wake, Damien Kandolo, alikuwa hayupo mara kwa mara na alikuwa akiitumikia serikali ya Ubelgiji kama jasusi. Lumumba alipokea uvumi kutoka kwa wapelelezi na maafisa wa usalama, jambo lililomfanya awe na wasiwasi mkubwa dhidi ya watu walio karibu naye. Ili kumsaidia kupata taarifa sahihi, katibu wake wa habari, Serge Michel, aliomba msaada wa waendeshaji telex watatu wa Kibelgiji waliompatia nakala za ujumbe wote wa waandishi wa habari waliokuwa wakitumwa nje ya nchi.

Lumumba alitoa amri kwa majeshi ya Kongo kuzuia uasi katika jimbo la South Kasai, ambalo lilikuwa na njia muhimu za reli kwa ajili ya kampeni dhidi ya Katanga. Operesheni hiyo ilifanikiwa, lakini mgogoro uligeuka kuwa ghasia za kikabila. Jeshi lilihusishwa na mauaji ya raia wa Luba. Wananchi na wanasiasa wa South Kasai walimshutumu Lumumba moja kwa moja kwa vitendo vya jeshi. Kasa-Vubu alitangaza hadharani kuwa ni serikali ya muundo wa shirikisho (federalism) pekee ingeweza kuleta amani na utulivu nchini Kongo. Hili lilivunja muungano wa kisiasa kati ya Kasa-Vubu na Lumumba, na kuhamisha ushawishi wa kisiasa kutoka kwa Lumumba aliyeunga mkono muundo wa serikali moja.

*Itaendelea toleo lijalo...*

# SAKO KWA BAKO:

## JALYNA MALOMBE — VITABU VIMENIJENGEA KUJIAMINI (MARUDIO)

JINA langu ni Jalyna Malombe, mtoto wa kwanza kwenye familia ya watoto watano, nikiwa wa kike peke yangu. Mimi ni Mmakonde wa Kitangali. Elimu yangu ya msingi nimesoma hapo Kitangali na Sekondari nimesoma Lindi Seko'.

Mi nimetoka katika familia ya kikulima, kwani baba yangu ni mkulima wa korosho ilhali mama yangu ni mama wa nyumbani. Baada ya masomo yangu ya Sekondari, baba yangu mdogo alinichukua na kunihamishia Dar es salaam. Yeye alikuwa anajivunia mimi kwa kuwa nimerithi jina la mama yao.

Baba yangu mdogo alikuwa askari wa jeshi la Magereza. Hivyo niliweza kuishi mikoa mbalimbali kadiri ya yeye alivyokuwa akihamishwa huku na huko. Hapa kwa baba mdogo ndipo nilipokutana na shelfu kubwa la vitabu. Kulikuwa na vitabu vya kila aina, yaani riwaya, mashairi, tamthiliya, vya dini na maarifa mengineyo. Yeye alipenda sana kusoma. Kila alipokuwa na nafasi ungemkuta na kitabu mkononi mwake.

**Kwahiyo tabia ya kusoma vitabu umerithi kwa baba yako mdogo?**

Ndiyo! Alikuwa ananisimulia hadithi nyingi sana za vitabuni kiasi kwamba nikaona wacha nizifaidi mwenyewe, ndipo nikaanza kusoma. Hii ilipelekea mpaka kugombana na mama yengu mdogo maana nilikuwa nasahau kufanya kazi.

**Hebu tuambie, wewe kwako vitabu vimekufanyia nini?**

Vitabu? Naweza sema wazi tu kuwa vitabu vilikuja kuwa mwalimu wangu mkubwa sana. Mi nilipokuwa kwa baba mdogo sikuwa nasoma na wala sikuwa nafikiri kusoma. Akilini mwangu nilikuwa na wazo moja tu kuolewa. Kuolewa, kuolewa, kuolewa… ni mawazo tuliyokuwa nayo wasichana wengi nyakati zile. Sasa kulikuwa na askari mmoja wa kike nilikuwa nampenda sana kiasi kwamba nikampa u-dada. Huyu alinishawishi sana kujiunga na jeshi la Magereza. Daima niliamini kuwa mwanamke hawezi fanya kazi za wanaume na ndiyo maana nilikuwa namshangaa sana huyu dada, namkumbuka alikuwa anaitwa Severina Severini, ila kwa sasa sijui alipo.

Kitabu kilichonipa mageuzi ya fikra kilikuwa ni Hawa The Bus Driver, uandishi wa Richard Mabala. Nikaona kumbe hata mwanamke anaweza kuwa hata dereva au zaidi.

Severina ndiye alimwambia baba mdogo kuhusu mimi kujiunga na Magereza. Hakukataa! Nikaandikishwa na kwenda Mbeya, Kiwila kwa mafunzo.

**Kwahiyo sasa wewe ni askari Magereza?**

Hapana, mimi si askari magereza, ila askari na kazi zangu nafanyia huku Songwe mpaka Tunduma ndiyo maeneo yangu.

**Je bado unapenda kusoma vitabu?**

Aisee, siwezi kuacha, kwangu imekuwa kama dini. Kwenye mkoba wangu hukosi kitabu hata ofisini wananishangaa sana.

Katika waandishi niliowasoma sana kwa nyakati hizi ni Eric Shigongo, vitabu vyake vilinibamba sana. Halafu Hussein Tuwa, kitabu Mkimbizi moto wa kuotea mbali. Halafu kuna huyu somebody Maundu yeye Kiswahili kwenye kazi zake ni shida.

Ila kiukweli mimi ni mpenzi sana wa Upelelezi na Ujasusi na uandishi wa Richard Mwambe na jeshi lake la Madam S ni hatari. Kutokana na kazi yangu riwaya za Kamanda Amata, Japhet Nyang'oro na nyingine nyingi zinanisaidia sana katika kutenda na kuamua kama askari.

**Asante sana Bi. Jalyna, basi nikutakie kazi njema. Japo bado tuna mengi ya kuzungumza na watu wajifunze…**

Asante sana, nashukuru kufikwa japo umenishtukiza. Karibu sana nina mengi ya kuzungumza



JALYNA MALOMBE

# MSALITI - 02

Na. Richard Mwambe

**Kitabu cha MSALITI sasa kinapatikana madukani. Jikamatie nakala yako uburudike.**

**Bei ni 15,000 tu. Wasiliana nasi kwa Whatsapp 0766974865.**

**Hawakufanya ukarabati wowote kwa kuwa kwa wao matundu hayo ya risasi labda yalikuwa maua ya kupendeza. Wanajeshi walikuwa kila kona ya eneo hilo, kuanzia hapo kwenye hilo jengo hadi huko kijijini ambako walihakikisha usalama wa wananchi wa Kongo ijapokuwa hawakukubaliana na kile kinachofanywa na Jeshi lao.**

***Endelea…***

Nje ya lile jengo palikuwa na bendera mbili kwenye milingoti yake; moja ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na nyingine ya Jeshi la nchi hiyo, FARDC. Aliteremka kutoka katika lile gari na kumwacha dereva aendelee na jukumu la kuliegesha vizuri. Alipokea salamu za kijeshi na kusindikizwa kuingia ndani ya lile jengo. Katika moja ya ofisi alikaribishwa na kuketi kwenye kiti kizuri cha magurudumu.

"Ripoti fupi!" akamwambia Askari kijana aliyekuwa amesimama mbele yake na kutengwa na meza moja kubwa kati yao.

"Vijana wamedhibiti misitu karibu yote ya Goma na Kivu, tunaendelea kuwarudisha nyuma waasi lakini wananchi wamekuwa kikwazo kikubwa sana…" yule Askari alieleza na kutulia huku akimtazama Jenerali Mathurin.

"Bado wanaendelea na ujeuri wao?" Mathurin akauliza kwa ukali.

"Ndiyo!"

Jenerali Mathurin akabaki kimya kwa sekunde kadhaa akiitafakari hiyo taarifa anayopewa. Kazi kubwa waliyotumwa ni kuwalinda wananchi wao dhidi ya waasi, lakini wananchi wenyewe wanalalamika kila uchao kuwa Jeshi hilo si lolote bora liondoke tu. Kauli hizi hazikumpendeza Mathurin hata kidogo kiasi kwamba ilifika wakati akawataka wananchi hao kuorodhesha majina ya wanajeshi wanaowanyanyasa. Wakafanya hivyo. Naye aliwarudisha wote kambini na kuomba wengine watiifu. Wengine hao walipofika haikuchukua hata miezi miwili malalamiko yakajirudia, tena kwa nguvu zaidi.

"Ok, nitakuwa na kikao Kinshasa, ngoja nikaendelee kusikiliza wakubwa wanasemaje, maana mambo hapa ni mengi," akamwambia yule Askari kijana. Naye akapiga saluti kisha akageuka na kuondoka kikakamavu. Alipohakikisha yule askari amepotelea nje, akainua simu yake ambayo ni dakika chache tu ilikuwa ikiunguruma kuashiria kuna ujumbe umeingia. Akaifungua na kuingia kwenye kikasha cha ujumbe mfupi.

'Kuna jambo muhimu la kuzungumza!

Fanya juu chini fika Beni kwenye hoteli yetu ileile…'

Ule ujumbe ulimwambia namna hiyo. Mathurin aliutazama na kuurudia kusoma mara kwa mara kabla hajaujibu. Alijua ni nini ambacho anaitiwa huko. Kutoka hapo alipo mpaka kufika Beni ingemgharimu saa nne au tano kwa barabara maana palikuwa na umbali wa kilomita mia mbili na tisini na tano tu. Kinachofanya kuwe na umbali wa saa tano hadi nne ni kutokana na ubovu wa barabara na misitu minene. Lakini isingekupasa kutumia muda mrefu kama ungekuwa unatembea kwenye lami, huku ukiwa na gari hiyo matata ya Kijapani.

*'Nina kikao Kinshasa kesho mchana,'*

Akajibu ule ujumbe.

*'Bosi wako anajua kila kitu, pita hapa tuzungumze,'*

*'Sawa!'* akajibu.

Jenerali Mathurin hakuwa na budi kuanza safari nyingine kuelekea huko Beni kwa njia ya barabara kupitia maeneo kama Bayonga, Lubero na Bulembo. Mara moja akainuka alipoketi na kutoka nje. Akamwita yule askari kijana ambaye

# MSALITI - 02



ndiye aliyekuwa anasimamia usalama wa Mweso akiwa na Jeshi la Serikali.

"Nitakuona baada ya siku nne, ila kama kuna jambo nitafute kwa simu yangu!" akamwambia kisha yeye akaingia garini, huku akimwacha yule askari bila maelezo ya ziada, naye kwa nidhamu ya kijeshi hakupaswa kuhoji hoji bali kutii agizo, 'Sawa Afande'.

"Tunaenda Beni!" akamwambia dereva wake mara baada ya kuketi kitini ndani ya gari lile na safari ikaanza mara moja.

❦

Ndani ya Hoteli ya Albertine katika Mji wa Beni, Kapteni wa jeshi la Kongo, Moise Kituli, alikuwa akimsubiri Jenerali Mathurin. Chupa ya Primus ilitulia mezani pake huku akitikisa mguu kufuatisha mirindimo ya muziki wa Lady Isa uliokuwa ukisikika kupitia spika maalumu ndani ya ukumbi huo. Hakuwa peke yake hapo ukumbini bali watu mbalimbali walikuwa wakila na kunywa. Ni yeye tu alikuwa peke yake katika meza hiyo aliyokuwa ameketi. Lakini kiti cha pili kilionekana wazi kuwa kinamsubiri mtu mwingine. Giza tayari lilishaifunika Beni, na kila wakati Kapteni Kituli alikuwa akiitazama saa yake ya mkononi. Saa nne usiku huo, Jenerali Mathurin aliwasili katika Hoteli ya Albentine na kumkuta mwenyeji wake. Yakafanyika maamkiano yaliyochukua kama dakika nzima hivi kisha naye aliitisha bia ya Castel baridi na kupoza koo.

"Pole kwa safari!" Kituli alimwambia.

"Nashukuru nimefika salama…" Mathurin akajibu huku akijinyoosha mwili wake pale alipoketi.

"Usalama upo sehemu zote ulizopita?" Kituli akauliza maana anafahamu hali ya misitu hiyo ya Kivu, huchelewi kukuta waasi wakiwa wamefanya yao au kuweka vizuizi njiani kila wanapoteka Kijiji.

"Kuko shwari, lakini kuna jambo moja linaniumiza kichwa sana!" akaweka shaka na kuonesha wazi kuwa hayuko sawa katika hilo.

"Shida nini?"

"Wananchi hawataki jeshi lao kuendelea kuwalinda, wanadai bado waasi wanafanya wanavyotaka, wanabakwa, wananyang'anywa mali zao na kadhalika… mimi kama kiongozi wa hii operesheni hainifurahishi maana najitahidi kadiri ya uwezo wangu," akaeleza. Jenerali Mathurin alisema hayo ingawa alikuwa na cheo kikubwa sana kuliko Kapteni Kituli lakini yeye aliamini ushauri hauendani na cheo cha mtu bali busara na mtazamo.

"Jambo zito sana hilo kamanda! Achana nalo we piga kazi… kwani wanaouawawa una nasaba nao?" Kituli akauliza. Jenerali Mathurin alibaki kumtazama tu. "Hii ni vita ya kimkakati… wewe upo jeshini na ni kiongozi mkubwa sana, lakini unaweza usijue hilo kutokana na kariba ya uongozi wako," Kituli akaeleza.

"Una maana gani?"

"Wakubwa wanajua, na walio chini yako wanajua… hii ni biashara afande, wakubwa wako wanatajirika kupitia hii vita. Hawa waasi wanawajua mpaka kwa majina yao na kuna maeneo ambayo unaona kabisa hatuwezi kuyakomboa kama jeshi hasa kwenye migodi, na si kwamba hatuwezi… waasi hawa wana nini cha kutuzuia sisi kuwatimua na kuwanyang'anya kila kitu? Lakini yote yamepangwa!"

Maelezo ya Kapteni Kituli yalimfanya Jenerali Mathurin kubaki kimya kabisa. Hakuwa na jibu la karibu, sembuse lile la mbali?

*Itendelea toleo lijalo...*

Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—01

MTUNZI: ASHA SIRAJ
Whatsapp 0789044345



***UTANGULIZI***

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhira**

***Twende nayo...***

Ilikuwa Jumatatu, siku ambayo sintoweza kuisahau kwenye maisha yangu. Na ni siku ambayo ilinifanya nianze kupitia magumu nikiwa bado nina umri mdogo sana.

Yalikuwa majira ya saa nane usiku ambapo harufu nzito ilisikika nyumba nzima. Wakati huo mama, baba pamoja na mdogo wangu Kavya walikuwa wamelala chumbani kwao.

Kipindi hicho nilikuwa na umri mdogo sana. Nakumbuka nilikuwa na umri wa miaka kumi, hivyo ilinibidi ninyanyuke nakutaka kujua hiyo harufu wapi inatokea.

Nilipigs hatua kidogo kuelekea sebuleni nikitafuta wapi inatokea harufu hiyo. Nilizidi kutumia pua zangu kunusa nusa kila sehemu.

Ndipo nilipogundua hiyo harufu inatokea jikoni. Basi, taratibu nilipiga hatua ndogo ndogo kuelekea jikoni, ila kilicho weza kunishangaza na kuniacha kinywa wazi ni pale nilipogundua gesi ilikuwa ikivuja kutoka kwenye mtungi mkubwa na kufanya kitu kama moshi ukiashiria unaka kuripuka.

Nilikimbilia chumbani kwa mama yangu kwa ajili ya kwenda kuwaamsha ili waweze kuifunga gesi hiyo kabla haijaleta madhara kwenye nyumba yetu.

Baada ya baba na mama kupata tarifa hizo walitoka kitandani haraka kuelekea jikoni mimi nikijaribu kuwafuata kwa nyuma ila mama alinikataza nakuniambia nibaki ukumbini wacha wao wafanye kazi hiyo.

Nilijaribu kuwabishia ila baba alinishika na kuniambia nikiwafuata basi atanipiga, hivyo ilinibidi nikae ukumbini kuwangojea.

Kelele kubwa ilisikaka jikoni ndipo nilipoweza kuona moto mkubwa ukitokezea huko wakati huo mlango wa jikoni ulijifunga. Niliogopa sana na kujikuta nikianza kulia nikiwa sijui nini cha kufanya. Nilianza kupiga kelele za kuomba msaada kwa majirani. Ila hakuna hata jirani aliyejitokeza. Sauti ya mama yangu ilisikika kwa mbali ikiniita. Kuna maneno alikuwa akiyaongea ila mimi sikuweza kusikia kutokana na moshi kuwa mwingi huku nikiwa nakohoa sana.

Nilifungua mlango wa nje usiku huo na kulekea nyumba ya jirani yetu kwa kwa ajili ya kuomba msaada ila mpaka nafika kwa jirani nyumba yote ilikuwa inawaka moto. Ndipo nilipokumbuka ndani kulikuwa na mdogo wangu amelala.

Nilirudi haraka ili niweze kumsaidia mdogo wangu ila moto tayari ulikuwa umeshika kila sehemu. Majirani walikusanyika pale wakijaribu kunizuia nisije kuingia humo ndani. Ila mimi sikuwa naelewa. Nilijaribu kulazimisha lakini wanilizuia kwa kunishika mikono. Hapo nikakosa namna ya kumsaidia mdogo wangu huku nikiwa sijui wazazi wangu wana hali gani humo ndani.

Nilipiga kelele sana ila kelele zangu hazikusaidia chochote. Hata kikosi cha Zima moto kilipowasili, bado sikuwa na uhakika hata wa kuwapata wazazi wangu kwasababu moto ulianza kuwaka muda mrefu sana. Mpaka muda huo walipowasili sikuwa na uhakika hata kama mifupa yao nitaiona au ndo majivu matupu.

Saa chache zilipita pasipo kupata majibu yoyote yale kuhusu wazazi wangu. Ilipotimu saa kumi na moja alfajiri, ndipo zoezi hilo la kuzima moto lilikamilika. Nilibaki kutumbua macho pale majirani walipoingia ndani nakutaka kujua kuhusu wazazi wangu.

Polisi nao walikwishawasili huku waandishi wa habari wakifutia nyuma wakitaka kujua chanzo cha tukio lote lililotokea mda mfupi kabla ya janga hilo

Waandishi wa habari walijaribu kunihoji pale, ila mimi kilio ndo kitu

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—01

kilichotawala kwenye macho yangu huku machozi mengi yakinitiririka kwa kama mto wakati wa masika.

Nilishindwa namna ya kuelezea tukio hilo hasa pale nilipogundua sipo nawazazi wala mdogo wangu tena! Hapo ndipo akili yangu ilizidi kuchanganyikiwa zaidi na zaidi.

Kilichoweza kupatikana ndani ilikuwa mifupa tu na wala sio miili. Hata mkono haukuonekana sembuse kichwa? Zaidi ni majivu na mifupa midogo midogo.

Nilipiga kelele za uchungu. Majirani walijaribu kunibembeleza pale ila mimi sikuwa naelewa na ukiangalia umri wangu ulikuwa mdogo, nisingeweza kufanya kitu.

Hatimaye kulikucha kabisa mimi sikuwa na amani wala furaha zaidi ya kilio tu. Nakumbuka mama hakuwa na familia zaidi ya baba pamoja na sisi watoto wake.

Nilijiuliza ni wapi nitaenda mimi, ikiwa sina bibi wala mama mdogo? Mtu aliyekuwepo alikuwa ni shangazi yangu Mariamu. Huyu ndiye mtu aliyekuwa ndugu wa pekee kwenye familia ya baba angu.

Mifupa ya wazazi wangu pamoja na mdogo wangu Kavya ilikusanywa kwa ajili ya kufanyiwa maziko. Niliumia sana. Yani ndani ya muda mchache sipo na wazazi wangu tena.

Nilifarijiwa ili niweze kuwa sawa , lakini ilikuwa ni sawa na bure tu. Maisha yangu yote nisingeweza kuishi bila wazazi wangu. Nilikuwa mtu wa kulia tu. Majira ya saa tatu asubuhi shangazi Mariamu aliwasili kutoka Dar es salam kuja nyumbani Morogoro, kwa ajili ya kufanya maziko ya wazazi.

Baada ya maziko kutamatika, ilibidi anichukue na kwenda kunieea maana sikuwa na ndugu zaidi yake. Hivyo sikuwa na budi. Nilikubali kwenda kuishi naye huko Dar es salaam. Tulikataka tiketi ya basi kwa ajili ya safari hiyo mimi na shangazi yangu. Bado nilikuwa mtu wa kulia tu, ila cha ajabu shangazi alionekana kutojari machozi yangu.

Alichoweza kusema ni kwamba nitalia hivi hadi lini, ikiwa wazazi wangu ndo kama hivyo. Alionekana mtu mwenye roho ngumu sana.

Baada ya saa chache tuliwasili jijini Dar es salaam, mpaka kinondoni alipokuwa akiishi shangazi. Alikuwa anaishi yeye pamoja na binti yake mmoja na mumewe. Binti yake kwangu alikuwa kama dada angu kwakuwa alionekana kunizidi kiumri.

Nakumbuka sikuwa hata na nguo wala kitu chochote mkononi zaidi ya zile nilizokuwa nazo kwenye tukio. Shangazi alionekana kuwa na maisha mazuri ila hakusubhutu kutoa hata hamsini mbovu ya kuniunulia nguo zaidi yakunipatia magauni ya binti yake ndo nivae.

Hayakujulikana kama ni magauni au kanzu, wala hakujali umri wangu niliokuwa nao. Zaidi alinipatia magauni makubwa yaliyonifanya niyashikilie mkononi kila nikitembea.

Kipindi hicho nilikuwa darasa la nne, kwa maisha yale niliyoyaona siku moja tu baada ya kufika kwa shangazi, ilionyesha dhahiri hapa dalili ya kusoma hakuna

✺

Ni mwezi mmoja umepita baada ya tukio la wazazi wangu kuanga dunia, nikiwa bado naishi na shangazi yangu. Nilikuwa kama mfanyakazi wa ndani. Shangazi aliniahidi kunisomesha ila sikuona dalili yoyote ile zaidi ya kutumikishwa tu.

Siku zilizidi kusonga mbele ndipo mume wa shangazi yangu alipoweza kunionea huruma nakuamua kunianzisha shule aliyokuwa akisoma binti yake.

Suala hilo lilimkera sana shangazi maana hakutaka kuniona nikisoma shule nzuri kama hiyo. Ndani yalikuwa marumbano kati yao, kwanini mumewe kanipeleka shule anayosomea binti yake.

Nilijijuliza sana hivi huyo shangazi amezaliwa tumbo moja na baba kweli au? Maana sio kwa roho mbaya aliyokuwa nayo.

Siku zilizidi kusonga mbele ni miezi sita sasa toka nianze kuishi na shangazi. Nakumbuka tulikuwa tukila shule huko huko, kama unavyojua chakula cha shule kilivyo wanafunzi ni wengi sana ila chakula nikichache.

Kiufupi sikuwa nashiba hivyo ilinilazimu nikirudi nyumbani basi walau niweza kupata chakula kingine, ila shangazi yangu hakuwa tayari kunipatia chakula.

***Itaendelea toleo lijalo...***



Mafuta yalipoanza kuchemka akalitoa kwenye jiko na kulipeleka uwani ilipo ile mitungi. Akafunua mtungi wa kwanza na kumimina yale mafuta ya moto kiasi cha kutosha, kisha kafanya hivyo hivyo katika kila mtungi.

Marjane akarudi jikoni na kumalizia kazi zake za kuandaa mboga ya kesho. Kisha akazima moto na taa.

“Leo siendi kulala,” alijisemea. “ Nitakaa hapa nione nini kitatokea.” Akakaa kwenye stuli karibu na dirisha akitazama uwani kwenye ile mitungi.

Kiongozi wa wezi alijilaza kitandani kwa muda na kusubiri. Alisubiri kwa muda mrefu sana. Baadaye akajisemea, “kwa muda huu kila mtu ndani ya nyumba atakuwa ameshalala.” Kisha akatoka kitandani na kuelekea dirishani, kisha kwa ukimya kabisa akafungua dirisha. Akaangalia uwani ilipo mitungi na kusikiliza. “Sioni taa yoyote,” alijisemea. “Na sisikii sauti yoyote, sasa nina uhakika kila mtu amelala humu ndani, na sasa ni hatua inayofuata ya mpango wangu. Nitarusha vijiwe kwenye ile mitungi, watu wangu wakisikia tu watatoka na kuanza mashambulizi kama tulivyopanga na kumkamata Alibaba!!”

Akachukua vijiwe alivyokusanya kabla ya kuja kulala na kuvijaza kiganjani na kuvirusha chini kwenye mitungi na akasikia sauti ya vijiwe vikiangukia kwenye ile mitungi. Alisubiri lakini hakuna chochote kilochotokea! Hakuna hata mwizi mmoja aliyetoka kwenye mtungi.

Kiongozi wa wezi akarusha tena vijiwe kiasi cha kujaza kiganja, vikaanguka tena chini na sauti akaisikia lakini kwa mara nyingine tena hakuna kilichotokea na wala hakuna jibu lolote.

Kiongozi wa wezi akaanza kuingiwa na woga sasa. Alihisi tu kuna kitu kimetokea.

Akawasha mshumaa na kushuka taratibu kulekea uwani kwenye ile mitungi yake, akafika kwenye mtungi wa kwanza kisha akafunua mfuniko kidogo.

“Uko tayari?” akauliza. “uko tayari kwa mapambano?” Hakuna jibu. Akajaribu kuvuta harufu. “nahisi harufu ya mafuta humu,” alijisemea. “mafuta ya moto!!”

Akafunua mfuniko wote na kuangalia ndani ya mtungi. Mwizi aliyekuwepo mle ndani ya mtungi alikuwa ameshakufa!!

Kiongozi yule wa wezi akaangalia katika kila mtungi kwa hasira na kukuta wezi wote wamekufa!

“Sijui nini kimetokea,” alifikiri. “Yaani watu wangu wote wamekufa, ina maana kuna mtu amegundua mpango wangu kwa kumshambulia Alibaba. Akaamua kuwaua! Sasa atakuwa nani kafanya hivi?? Alibaba mwenyewe?? Mke wake?? Oooh siko salama tena kwenye nyumba hii yaani nimebaki peke yangu, lazima nikimbie kuokoa maisha yangu.

Kiongozi wa wezi akaacha mitungi yote na punda wote na kuruka kwenye ukuta wa uwani, akakimbia mbio zote kwa kadiri awezavyo. Lakini hakumsahau Alibaba. Alikuwa na hasira sana na bado alihitaji kumuua.

Asubuhi iliyofuata, Alibaba aliamka mapema sana, akachukua taulo yake na sabuni. Kisha akashuka chini na kukuta mitungi ile bado ipo.

“Ajabu! Hii mitungi bado ipo hapa sasa hivi” alijisemea. “Lakini bado mapema sana labda muuza mafuta bado amelala.”

Kisha Alibaba akaondoka kuelekea bafuni. Hakujua lolote lililotokea usiku ule.

Alibaba alipotoka bafuni bado aliiona mitungi ile arobaini pale uwani na muda ulikuwa umeenda kidogo, akilinganisha kauli ya mgeni wake kwamba angeondoka asubuhi sana kuelekea kwenye safari yake ya kuuza mafuta.

“Marjane!” Alibaba aliita, “Mbona muuza mafuta bado hajaondoka?”

Marjane akatoka jikoni. “Nitakuelezea kila kitu bosi wangu.”Marjane alisema. “Lakini kwanza hebu angalia ndani ya mitungi hiyo.”

Alibaba alichanganyikiwa kidogo kusikia hivyo. Akasogea na kufunua mfuniko wa mtungi mmoja.

“Kuna mtu humu!” alisema kwa mshtuko. “Tena amekufa!!”

Aliangalia katika kila mtungi. “Watu thelathini na tisa waliokufa ndani ya mitungi na mtungi mmoja una mafuta kidogo! Kumetokea nini Marjane?”

“Kuna mtu anajaribu kukuua, bosi,” Marjane alijibu. “Kuna siku niliona alama nyeupe ya chaki kwenye mlango wa mbele wa nyumba yetu.

***Itaendelea toleo lijalo***

# TUCHAWA Yaupa Heshima Ushairi Nchini

KWAKO itakuwa ni jina geni sana 'TUCHAWA', ndiyo ni geni kwa kuwa ni mara ya kwanza kusikika hadharani.

TUCHAWA ni kifupisho cha Tuzo za Ushairi CHAguo la WAsomaji. Hii ni tuzo iliyoandaliwa na wadau wa ushairi nchini kwa mara ya kwanza hapa Tanzania. Tuzo hii iliyokusudiwa kuwatambua washairi nchini ilifanyika mwezi wa Machi, tarehe 21 sambamba na Siku ya Ushairi Duniani.

Waswahili wanasema 'Mwanzo wa Ngoma ni Lele'. Hakika TUCHAWA imedhamiria kuonesha thamani ya ushairi na washairi katika ukanda wa Afrika Mashariki kwani Tuzo hizi zilipokea miswada hata kutoka nchi jirani ya Kenya.

Katika hali isiyotegemewa, washiriki kutoka Kenya wamejinyakulia nafasi ya kwanza katika kipengele cha Mshairi Bora Chipukizi wa Mwaka 2024—2025 iliyochukuliwa na Chipukizi Ally Mwakaga. Ushiriki wa washairi kutoka Kenya kwenye Tuzo hii umeonesha taswira ya nini TUCHAWA inataka kufanya katika tanzu hii ya fasihi.

Hisia ziliuteka ukumbi mara baada ya kutangazwa mshindi wa Shairi Bora la Mwaka, Jane David Mwanizuwa. Mwanamke huyu aliyezaliwa mwaka 1996 amekuwa kivutio kikubwa cha wapenda fasihi kwa umahiri wake wa uandishi kwenye riwaya na mashairi. Umahiri wa 'kalamu' yake umemfanya kuwa rafiki kipenzi cha wengi. Yeye daima hutumia kitimwendo kutokana na hali aliyonayo. Lakini pamoja na hali hiyo na ile ya kupoteza uwezo wa kusikia bado hajaona kuwa hayo ni ya kumkatisha tamaa, anapambana, anaandika na amekuwa bora sana.

Katika hotuba yake Mgeni Rasmi Mh. Nyambari Nyangwine alitoa 'somo la bure' kwa wshairi wa kisasa wanaoghani na kutunga ushairi usiozingatia vina na mizani akiwataka kujikita katika asili ya ushairi. Vilevile aliahidi kuaandaa semina maalum ya utunzi wa ushairi kwa walioshiriki Tuzo hiyo na wengineo kwa minajiri ya kuwanoa zaidi kwa kuwatafutia waalimu mahiri watakaoendesha semina hiyo. Aliendа mbali zaidi na kusema kuwa yuko tayari kuchapa vitabu vya ushairi ambavyo TUCHAWA itaandaa baada ya semina hiyo kufanyika.

Uwepo wa Mh. Nyambari Nyangwine katika usiku ule ilitoa taswira pana ya wapi TUCHAWA inalenga kufika. Pamoja na mgeni rasmi pia alikuwapo mwakilishi wa Ubalozi wa India. Kama mwalikwa.
Usiku wa TUCHAWA uliofanyika Ngome Holdings pale Sinza, Jijini Dar es salaam uliwakutanisha mashabiki, wapenzi na wadau wa fasihi. Pamoja nao walialikwa waandishi wa riwaya bunifu ambao uwepo wao ulidhirisha umoja uliopo katika fasihi na wanafasihi wa Kiswahili. Wachache kati ya waliokuwepo ni pamoja na Hussein Molito ambaye ni Mkurugenzi wa Kalamu Tulivu na Mariam Mbano Mkurugenzi wa Marm'z Relation Hub ambao walikuwa sehemu ya wadhamini wakubwa wa tukio hilo. Frank Masai mmiliki na mwasisi wa jarida pendwa la Kifasihi la Tulizo, Amata Ric Mkurugenzi wa NGO ya Kitabu Maisha, Eva Mrema 'Kungwi', Hussein Wamaywa Mkurugenzi wa TAFF, Goima Mkurugenzi wa Mtalimbo Books na wengineo wengi.

Achilia mbali Tuzo hizo, washiriki wote walipata nafasi ya ku-futuru pamoja ikiwa ni alama ya kuutukuza Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

**ORODHA YA WASHINDI**

1. Mshairi Bora Chipukizi wa Mwaka 2024—2025 ni Ally Mwakaga kutoka Kenya.
2. Mshairi Bora wa Mwaka 2024-2025 ni Shaban Athumani Maulid
3. Mshairi Bora wa Kike 2024—2025 ni Sharifa Mohamed Ally
4. Kundi Bora la Mwaka 2024—2025 ni Tungo Zetu na Mwana wa Tanga
5. Shairi Bora 2024—2025 ni Jane David Mwanizuwa

# HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—02

Katika mwendeleo wetu wa Historia ya Vitabu Duniani, toleo lililopita tuliona historia fupi na kuanza kuchambua vitabu vya kale. Katika toleo lile tulipitia kitabu cha EPI OF GILGAMESH kama ifuatavyo:-

1. **Epic of Gilgamesh** (karibu 2100 KK) – Hiki ni moja ya maandiko ya kwanza kabisa katika historia, kilichoandikwa kwa maandishi ya msumari kwenye vibao vya udongo huko Mesopotamia (Iraki ya sasa).
Katika toleo hili tunaendelea na kitabu kingine KITABU CHA WAFU.

## 2. Kitabu cha Wafu (Book of the Dead)

Kitabu cha Wafu *(Book of the Dead)* ni mkusanyiko wa maandishi ya kidini ya Wamisri wa kale, yaliyokusudiwa kusaidia roho za wafu kupitia ulimwengu wa akhera na kufanikisha maisha ya milele. Jina hili linatokana na tafsiri ya Wazungu (hasa Wajerumani) waliogundua maandiko haya karne ya 19, lakini jina halikuwa la asili ya Wamisri.

**Maelezo Muhimu kuhusu Kitabu cha Wafu:**

**1. Asili yake:**
- Kilianza kuandikwa takribani mwaka 1550 KK hadi 50 KK.
- Ni mkusanyiko wa nyimbo, dua, maagizo na matamshi ya kichawi.
- Kiliandikwa kwa maandishi ya *hieroglyphics*, *hieratic* au *demotic*.
- Mara nyingi kiliandikwa kwenye *papyrus*, na kuwekwa ndani ya kaburi pamoja na marehemu.

**2. Kusudi lake:**
- Kumsaidia marehemu kuelewa kinachotokea baada ya kifo.
- Kumpa mwongozo wa kuvuka vizuizi vya dunia ya wafu.
- Kuandaa roho ya marehemu kwa ajili ya hukumu ya mwisho – ambako moyo wake unalinganishwa na manyoya ya *Ma'at* (mungu wa haki na utaratibu).
- Kuimarisha nafasi ya marehemu kufikia Bustani ya Aaru (paradiso ya Wamisri).

**3. Maudhui Muhimu Ndani Yake:**
- Tamko la kutokuwa na hatia *(Negative Confession)*: Marehemu anasema dhambi ambazo hakufanya ("Sikuiba," "Sikuua," "Sikumwambia mtu uongo," n.k.).
- Mazoea ya kichawi: Matamshi ya kuwatuliza majini, kuzuia mitego, na kupata ulinzi kutoka kwa miungu kama Osiris, Anubis, na Ra.
- Maono ya Akhera: Maelezo ya maisha ya baada ya kifo, hukumu, na safari ya roho.

**4. Miungu Muhimu:**
- Osiris – mungu wa wafu na ufufuo.
- Anubis – mungu wa uimbaji wa wafu na mlinzi wa makaburi.
- Thoth – mungu wa hekima, mwandishi wa hukumu.
- Ma'at – mungu wa ukweli na haki.

**Mifano ya Vifungu maarufu:**
Tamko la Haki (kutokuwa na hatia):
"Sikutenda dhambi dhidi ya mtu yeyote. Sikuiba. Sikufanya uzinzi. Sikusema uongo..."

**Dua ya kuamsha roho:**
"Ee roho wangu, usinishuhudie kwa uovu mbele ya mahakama ya miungu..."

Unapovutiwa na Kitabu cha Wafu, unaweza pia kulinganisha na maandiko mengine ya kale kama vile:
- The Tibetan Book of the Dead (Bardo Thodol)
- Divine Comedy ya Dante (karne ya kati)
- The Epic of Gilgamesh (kwa maudhui ya maisha na kifo)

Katika toleo lijalo tutaendelea na makala hii ya historia ya vitabu ulimwenguni.

Muwe na sikukuu njema!

***Itaendelea...***

## Utangulizi

Kitabu cha Atomic Habits kilichoandikwa na James Clear kimekuwa chenye kubadilisha maisha ya watu wengi sana na kinatoa mwanga juu ya nguvu ya mabadiliko madogo katika kuunda tabia zetu za kila siku. Kitabu hiki kinajikita katika wazo la jinsi maboresho madogo na ya mara kwa mara yanavyoweza kuchangia mafanikio ya muda mrefu.
Mwandishi anasisitiza kwamba badala ya kuzingatia mabadiliko makubwa, tunapaswa kuwekea mkazo wetu kwenye athari ya mabadiliko madogo ya tabia.

Kitabu cha **Atomic Habits** kinatufundisha Sheria Nne za Tabia - ikiwa ni pamoja na kuifanya iwe ya kila siku (mazowea); kuifanya iwe ya kuvutia; kuifanya iwe rahisi; na kuifanya iwe ya kuridhisha.
Leo nakuletea baadhi ya mafunzo nane (8) kutoka kwenye kitabu hiki. Nayo ni

**1. Boresha 1% Kila Siku**

Watu mara nyingi hujaribu kuchukua hatua kubwa zaidi kuliko wanavyofanya kawaida. Mara nyingi hii husababisha kushindwa njiani. James Clear anaonyesha kwamba kuboresha nafsi yako kwa 1% kila siku kutakuwa na athari kubwa kwa utu wako na tabia zako kuliko kuchukua hatua kubwa mara moja kwa mwezi.

**2. Tabia Zako Ni Kioo Cha Utambulisho Wako**

Ni muhimu kuelewa kwamba tabia zako si kitu cha kujificha. Tabia zako ni kioo cha utambulisho wako. Mwandishi amesema usijilazimishe kuwa na tabia ya kusoma vitabu 30 kwa mwaka au kuandika makala 10 katika miezi 10. Bali unatakiwa kuweka tabia ya kuwa kuwa msomaji au "kuwa mwandishi mzuri na meendelevu. Ukiwa ktk hali hii utaelekeza umakini wako kwa mapana na picha kubwa zaidi.

**3. Mzunguko wa Tabia *(habit loop)***

Kitabu hiki kinaeleza mzunguko wa tabia wenye hatua nne ambazo ni:
Ishara, hamu, majibu na Zawadi.
Ili upate zawadi lazima kuwe na kitu kinachoashiria wewe kuweza kujiingiza. Ukijiingiza utaanza kupata hamu hamu itakupelekea kupata majibu ya kile unachokitafuta na mwisho utakipata kama zawadi.

**4. Furahi sasa, usingoje baadaye**

Watu wengi huacha kitu kinachowafanya wasiwe na furaha sana. Mathalan, ikiwa unaanzisha biashara ili kupata pesa lakini ghafla ukakutana na changamoto nyingi, utaacha. Kwa nini? Kwa sababu unategemea furaha yako kwenye matokeo unayotaka kufikia, na unaposhindwa kuyapata, unakata tamaa.

**5. Muendelezo *(consistency)* ni kitu muhimu**

Dhana ya kuboresha nafsi yako kwa 1% kila siku inategemea muendelezo wako. Kushikilia tabia mpya hakuhusiani na muda, bali ni kuhusu jinsi unavyofanya mara kwa mara. Ikiwa utakuwa na muendelezo thabiti, utafanikisha lengo lako.

**6. Kitu kidogo ni bora kuliko kukosa kabisa**


Kujenga tabia za kudumu si kila wakati kunahusu kuchukua hatua kubwa. Kufanya kitu kidogo mara kwa mara na endelevu bora kuliko kufanya jambo kubwa kwa kutokuwa na muendelezo *(consistence)*. Mathalan, kusoma kurasa 2 za kitabu kila siku ni bora kuliko kusoma kurasa 10 kila mwezi. Hivyo, kuwa na busara katika kuchagua tabia zako unazotaka kujijengea kwa kuanza "kitu kidogo" kuliko "kila kitu."

**7. Tabia zako za sasa zina msaada mkubwa kwako**

Hii inaitwa kufunga tabia *(habit stacking)*. Inamaanisha, tumia tabia zako za sasa kujenga tabia mpya. Hii ni njia bora zaidi ya kushikilia tabia zako.

**8. Tafuta wa kushirikiana naye, usifanye peke yako**

Kuwa na mshirika wa kufanya kazi pamoja katika tabia zako ni bora kila wakati kwani inakusaidia kubaki kwenye malengo yako. Kwa mfano, mnaweza kuhamasishana kwenda kukimbia pamoja au kwenda *gym* pamoja. Ikiwa utakuwa peke yako, huenda usijisikie kufanya hivyo, lakini unapokuwa na mwenzako kunaweza kukusukuma kufanya bora zaidi.







Picha Za usiku wa TUCHAWA









TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.
Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.
Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com

## NAWAPONGEZA

Shindano kutolibeza
Ushindi mulitaraji
Ndipo mkajitokeza
Chaguo la Wasomaji
Vigezo mliviweza
Waloviweka majaji
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

Kupambana mmeweza
Hadi kunyaka mataji
Watu muliwachombeza
Kura mkizihitaji
Kutwa mkawahimiza
Vitambulike vipaji
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

Kwanza ni weye Sharifa
Malenga ulobobea
Tungo zenye maarifa
Watu walijionea
Bila chembe ya kashifa
Kileleni umekwea
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

Naweye bwana Shabani
Tuzo umeipokea
Ni kwa ujuzi wa fani
Hawaja kupendelea
Umeshinda hadharani
Tuzo uloigombea
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

Piya Mwakaga wa Ali
Mshairi chipukizi
Watu wamekukubali
Kwa kipaji na ujuzi
Kura umepata kweli
Pasipo na ubaguzi
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

Dada Jane Mwanizuwa
Nani kasema huwezi
Ushairi waujuwa
Mola kakupa mbawazi
Umma umeushituwa
Pamwe kupata waazi
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

Tama ni mwana wa Tanga,
mshindi wa kundi Bora.
Ingawa bado mchanga
kazizo zina ubora
Watunga si kubanga
ndipo ukatia fora
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

Hizi ni pongezi kwenu
Msambe n'nahambara
Ushindi ni haki yenu,
Watoaji ni hadhira
Mtunze vipaji vyenu,
Ja msingi na tijara
Mlioshinda Tuchawa
Washindi nawapongeza

**DARUWESHI MKULU WANYIKA**
**MWENESESEME NOGAYA WA SABA (VII).**
**MAGOMENI MWEMBECHAI, DAR ES SALAAM**

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# TANGAZO













Jenga tabia ya kusoma vitabu kila upatapo muda. Vitabu vyetu vinapatikana

Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni - Simu namba 0655428085
Posta Mpya Dar es salaam karibu kabisa na mzunguko wa Sanamu ya Askari kwa Joji - Simu 0713454152
Morogoro Morena hotel, Stendi ya Dalala Smaki Samaki na Bima kwa Markus Mpangala - Simu 0719226293
Au wasiliana nasi Jamvi la Simulizi kwa Whatsapp Namba 0766974865

# KUTOKA MAKTABA: MAISHA NI MAPAMBANO—8

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

## TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA—7

### SURA YA 3
### Kisomo na maendeleo kijijini

Mpepo: Mbona nakunywa nao pombe siku zote hawajanipa kazi?
Luzolo: Uliwaambia kama unahitaji kazi?
Mpepo: Hapana lakini wanajua kama sina kazi.
Luzolo: Kwani ndugu zako?
Mpepo: Hapana marafiki tu.
Luzolo: Wasiwape kazi jamaa zao wakupe wewe bila hata kuomba hiyo ni akili? (Alimzindua)

Mpepo aliduwaa kwa maneno ya mkato ya rafiki yake, lakini yenye maana nzito. Kabla hajasema chochote alimwomba sigara avute. Luzolo akamwambia "Nasikitika ilikuwa moja tu ambayo nimeimaliza sasa hivi, si umeona mwenyewe?" Mambo yanazidi kuwa mabaya zaidi upande wake, alisononeka. Akaamua kuondoka na kwenda zake, lakini hajui aende wapi; si nyumbani. Hata hivyo Luzolo alisisitiza kwamba akawaambie marafiki zake hao huenda wakampatia kazi na sipuuze ushauri huo. Akaondoka moja kwa moja hadi kilabuni anakonywea pombe.

Kama kawaida aliwakuta marafiki zake. Hakuwa amechangamka kama desturi yake. Walimkaribisha na kuanza kunywa. Punde si punde akatumwa kumtafuta mwanamke fulani alete pombe nyingine. Akaenda bila kucelewa maana hii ndiyo kazi aliyoizoea. Akamleta mama mmoja ambaye siye waliyemhitaji. Kwa pamoja wakamsakama "Siye huyu Mpepo". Mpepo akawaambia kuwa yule wanayemhitaji hakuwepo siku ile. Lakini waliendelea kumshutumu; kwamba ingefaa arudi na sio kusema na kuleta ghasi nyingine. Hayo yote na yale aliyokuwa nayo kichwani yalimpunguzia raha. Alipiga moyo konde kwa vile alikwishakata shauri kuwaelezea shida yake ya kazi.

Kikao kiliendelea. Baada ya kuona kila mmoja alikuwa na furaha ya kutosha—kabla ya kulewa, alitoa dukuduku lake huku akitaja baadhi ya matatizo yake ya nyumbani. Walimhurumia, lakini mmoja akamcheka na kumuuliza ya kuwa siku zote alikuwa wapi. Aliwafahamisha kwamba siku za karibuni tu kuliandikwa wafanyakazi wengi kazini kwake. Mwisho aliulizwa ni kazi gani angependa. Akajibu kazi yoyote maana hakuwa na kisomo kikubwa wala ujuzi. Hicho kisomo cha zamani pia kilikuwa kinamtoka polepole. Akaambiwa asubiri majuma mawili. Ghafla Mpepo akaanza kupata nguvu na furaha mpya. Alikuwa kama mtu ambaye amekwishaajiriwa kazi.

Majuma mawili hayakupita, Mpepo aliajiriwa kazi ya utarishi katika ofisi ya mifugo. Pamoja na kuajiriwa kwake maisha hayakuwa mazuri sana maana alijiingiza kwenye majanga mengine ukiwemo uasherati, ulevi wa kupindukia na kushindwa kuachana na marafiki zake ambao walimsaidia kupata kazi. Wao walikuwa na kipato kikubwa kuliko yeye, lakini lazima ashindane nao kutoa oda.
Baada ya kuona hakuna alichokuwa anapata kutokana na kazi yake, aliamua kuacha kazi ya utarishi. Walishikamana na mama Tabu katika kuendeleza kilimo shambani kwao.

Ofisi ya mifugo ilipata pengo kubwa Mpepo alipoacha kazi. Alikuwa hodari wa kazi, mtiifu na mwepesi. Aliwahi kupigiwa majungu kwa uhodari wake. Wengine walimwita kibaraka wa meneja na wengine walimwona kama anawachafulia kazi. Msimamo wake ulikuwa kwamba. Kutegea kazi kulikuwa na maana wakati wa ukoloni. Kutegea au kugomea kazi kulidhoofisha uwezo wa mkoloni tofauti na itikadi ya hivi sasa katika nchi yetu.

***Itaendelea toleo lijalo….***

SOMA VITABU
- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE
- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI
- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vitabu
- Kupiga stori na waandishi

# MABADILIKO YA TABIA NCHI NI NINI?

Mabadiliko ya tabia nchi ni mabadiliko ya muda mrefu katika hali ya hewa ya dunia, hasa joto, mvua, na hali zingine za hewa, ambazo husababishwa na shughuli za binadamu pamoja na sababu za asili. Kwa kifupi, ni hali ya dunia kubadilika kwa namna isiyo ya kawaida kutokana na kuongezeka kwa gesi chafuzi kama vile kaboni dayoksaidi ($CO_2$), ambayo husababisha ongezeko la joto duniani — jambo linalojulikana kama *(global warming)*.

## Sababu kuu za mabadiliko ya tabia nchi ni pamoja na:

1. Uchomaji wa mafuta ya kisukuku (kama makaa ya mawe, mafuta ya petroli, na gesi asilia) kwa ajili ya uzalishaji wa umeme, viwanda, na usafiri.

2. Ukataji wa miti hovyo, unaopunguza uwezo wa miti kufyonza kaboni dayoksaidi.

3. Kilimo na mifugo ambayo huchangia uzalishaji wa gesi za methane na nitrous oxide.

4. Matumizi makubwa ya nishati na bidhaa zisizo rafiki kwa mazingira.

## Madhara ya mabadiliko ya tabia nchi ni pamoja na:

Kuongezeka kwa joto duniani.

Mafuriko na ukame wa mara kwa mara.

Kiwango cha bahari kuongezeka.

Kuyeyuka kwa barafu maeneo ya aktiki na antaktiki.

Kuongezeka kwa magonjwa na changamoto za chakula.

Uharibifu wa mazingira na kupotea kwa viumbe hai.

## Tunaposema uchomaji wa mafuta ya kisukuku twamaanisha nini?

Uchomaji wa mafuta ya kisukuku ni moja ya sababu kuu za mabadiliko ya tabia nchi. Mafuta haya ni makaa ya mawe, mafuta ya petroli, na gesi asilia, ambayo yamehifadhiwa ardhini kwa mamilioni ya miaka kutokana na kuoza kwa viumbehai waliokuwepo zamani.

**Hii hapa ni namna uchomaji wa mafuta ya kisukuku unavyochangia mabadiliko ya tabia nchi:**

**1. Uzalishaji wa gesi chafuzi**

Wakati mafuta ya kisukuku yanapochomwa, huachilia gesi kama:

Kaboni dayoksaidi ($CO_2$)

Methane ($CH_4$)

Nitrous oxide ($N_2O$)

Gesi hizi hujikusanya kwenye angahewa na kutengeneza tabaka linalonasa joto la jua — kama "blanketi" — linalosababisha joto duniani kuongezeka *(greenhouse effect)*.

**2. Matumizi ya kila siku yanavyochangia**

Usafiri: Magari, ndege, na meli nyingi hutumia petroli au dizeli — vyote vinachomwa na kutoa gesi chafuzi.

Umeme: Nchi nyingi bado hutegemea makaa ya mawe au gesi asilia kuzalisha umeme.

Viwanda: Sekta ya viwanda huchoma mafuta kwa uzalishaji, hasa katika kutengeneza chuma, saruji, plastiki, n.k.

**3. Athari zake kwa mazingira**

Kuongezeka kwa joto la dunia.

Kuyeyuka kwa barafu maeneo ya baridi.

Kuongezeka kwa kiwango cha bahari.

Mabadiliko ya mvua (mvua kubwa kupita kiasi au ukame).

Kuongezeka kwa vimbunga, mafuriko, na majanga ya asili.

**4. Suluhisho na mbadala**

Nishati mbadala: Kama vile jua, upepo, na maji (hydro).

Kuongeza ufanisi wa nishati: Kutumia vifaa vinavyotumia umeme kidogo.

Kupunguza matumizi ya magari ya mafuta: Kutumia magari ya umeme au baiskeli.

Upandaji wa miti: Miti husaidia kufyonza $CO_2$.

**Tangazo la Umoja wa Mataifa**

Umoja wa Mataifa (UN) umetangaza wazi kuwa mabadiliko ya tabianchi ni moja ya changamoto kubwa zaidi za wakati wetu. Kupitia taasisi zake kama UNFCCC (United Nations Framework Convention on Climate Change), IPCC (Intergovernmental Panel on Climate Change), na vikao kama COP (Conference of the Parties), UN imetoa msimamo na hatua mbalimbali kuhusu suala hili. Kwa ujumla, Umoja wa Mataifa unasema:

Mabadiliko ya tabianchi yanatokana na shughuli za binadamu. Ripoti za IPCC zinaonesha kuwa ongezeko la joto duniani linasababishwa kwa kiasi kikubwa na uzalishaji wa gesi chafu (kama $CO_2$ na methane) kutokana na matumizi ya nishati ya mafuta, kilimo, ukataji miti, na viwanda.

Athari zake ni mbaya na zinahatarisha maisha. UN inasema mabadiliko ya tabianchi yanasababisha majanga kama mafuriko, ukame, moto wa misitu, kuongezeka kwa kina cha bahari, na kuyeyuka kwa barafu. Haya yote yanaathiri chakula, maji, afya, na makazi ya watu.

Hatua za haraka zinahitajika. UN inasisitiza kuwa dunia lazima ipunguze haraka uzalishaji wa gesi chafu na kuhamia kwenye nishati safi kama vile umeme wa jua, upepo, na vyanzo vingine visivyochafua mazingira.

**Mkataba wa Paris (Paris Agreement)**

Umoja wa Mataifa uliratibu mkataba huu mnamo 2015, ambapo nchi zaidi ya 190 zilikubaliana kuweka mipango ya kudhibiti joto lisizidi nyuzi joto 1.5°C – 2°C juu ya viwango vya kabla ya mapinduzi ya viwanda.

**Haki ya mazingira kwa wote:** UN inasema vita dhidi ya mabadiliko ya tabianchi vinapaswa kufanyika kwa haki, kwa kuhakikisha kwamba mataifa yaliyoathirika zaidi (hasa ya Afrika, visiwa vidogo na mataifa yanayoendelea) yanasaidiwa kifedha na kiteknolojia.

**Ushirikiano wa kimataifa ni muhimu:** Umoja wa Mataifa unasema hakuna nchi itakayoweza kutatua tatizo hili peke yake. Hivyo, ushirikiano wa kimataifa, ushiriki wa sekta binafsi, jamii na vijana ni muhimu sana.

**TANGAZO**



## HAPPY NEW YEAR '04'—Twahir Yusuph

**Ilipoishia...**

***(Shit).*** **Sauti hiyo simuni ikaonesha kama kusikitishwa na taarifa hiyo anayoitoa. *"SO SAD, NIMEHUZUNISHWA SANA RAFIKI YANGU CHIDI."* simu ikakata.**

***Endelea...***

Nani angeweza kuvumilia, nani ambaye angekuwa mstahimilivu kwa hiki cha pili anachokisikia CDF Rashidi Koboko?
Ni nani huyo mwenye moyo mgumu wa kulipokea na hili kisha akashukuru kirahisi kabisa? Kwa mara ya nyingine simu ilimdondoka mkuu wa majeshi nchini. Kiwepesi sana sauti ya muuaji imempa taarifa mbaya kumhusu mkewe. Katikati ya hii nyingine inayozitisha mboni zake muda huu. Hili ndilo pigo takatifu la huzuni, alilolipokea akiwa kileleni mwa uchungu mwingine alioshindwa kukabiliana nao. Afanye nini? Alie labda utapoa? Hapana. Kwanza ataamini vipi kama alichoambiwa ni cha kweli! Akiwa yupo ardhini mwa bahari ya majonzi na mawazo pamoja, simu yake inatetema tena CDF Rashidi Koboko, aliyageuza macho yake yatiririshayo machozi na kuitazama. Ilikuwa jumbe kutoka namba aliyoihifadhi kwenye simu yake, ni Rais wa nchi yake ya TAKASENI profesa Omar Kifaranga.

Kinyonge sana aliikamata tena na kuifungua jumbe hiyo, *Pole sana kwa vifo hivi viwili vya kushtukiza rafiki yangu, Mungu awe upande wako katika kipindi hichi kigumu. Ningekupigia ila nafahamu hali uliyonayo kwa sasa.* Jumbe ilieleza hivyo. Atake nini tena ili kimuaminishe? Amepoteza mke na mtoto kwa mkupuo, tena kwa vifo vya kusababishwa na mtu aliemuonesha wazi unyama alioufanya.

Uchungu ulimtafuna akisononeka na kulilia nafsini hadi machoni, maumivu aliyoyahisi ndani ya chumba hicho cha mochwari aliyajua yeye na Mungu wake, hata vijana wake walibaki wakikishangaa kilio chake. Alilia kama mtoto CDF Rashidi Koboko. Wanajeshi wake wawili hawakua na chaguzi ya kufanya, wanasema kumwaga machozi yanayokuumiza ni tiba pia. Walimwacha aipoze huzuni yake hadi itakapompa japo afueni, watamsaidia.

* *

Nini kimelikumba Taifa la Takaseni? Nini kusudio la mauaji hayo? Ipi maana ya neno "HAPPY NEW YEAR" alitumialo muuaji kila akitekeleza azimio lake hilo baya na la kutisha?

Zile saa 48 alizozitoa IGP Edward Kituo kwa jeshi lake la polisi, zilitimia na kutokomea bila jawabu walilolitaka. Zilipita na kum'bakishia muuaji uhuru wake, akiendelea kula anavyovitaka huko aliko. Wataalamu wa kimtandao pia bado hawakuweza kubaini chochote, dhidi ya kurasa hiyo ovu inayotishia amani, na kuiwewesesha mno nchi yao.

Misiba ilitamatishwa, Jax na Imraan wote walishasitiriwa kwenye mashimo yenye jina la kaburi, hata mke kipenzi wa CDF Rashidi Koboko, naye alishahifadhiwa kwenye nyumba yake ya milele. Watoto wa wakuu hao wawili kutoka vitengo nyeti kabisa vya nchi, pamoja na mke mmoja, waliacha maswali mengi ya ukakasi kwenye vichwa vya wananchi na serikali.

*****

Majira yakapishana na kuzikimbiza zile nyakati mbaya zilizowakumba. Ni siku ya tano sasa tangu majonzi yafanye ziara yake ndani ya familia hizi kubwa nchini. Leo kiliitishwa kikao, mada ikiwa ni namna gani ya kumtia nguvuni mhalifu aliyejitokeza kusikojulikana siku chache zilizopita, na kuwaletea zawadi za misiba wasiyomuagiza.
Ndani ya ikulu iitwayo MWEWE, sehemu anapoishi Rais wa nchi yao ya Takaseni. Meza ndefu na ghari ilizungukwa na suti chache pamoja na sare za askari polisi wengi wa vyeo vya juu. Pia akiwepo na mkuu wa jeshi la ulinzi na usalama Bwana CDF Rashidi Koboko. Viti vyote pahala hapo viliibeba miili hai ya vongozi wa ulinzi na usalama wa nchi tu, hadi na waziri wake. Sura zao hazikuwa na mzaha. Kila kinywa kiliidadavua mada iliyowekwa mezani. Wanampata vipi muuaji? Muafaka ukapatikana, jukumu likaachwa kwa jeshi la polisi, likiongozwa na mwenyewe IGP Edward Kituo, pamoja na mkuu wa masuala ya kipelelezi na makosa ya jinai bwana Alfred Chigamba.

"Namuamini sana, na nina hakika kazi hii ataifanya ndani ya muda sahihi, na inavyotakiwa." Alfred Chigamba aliongea huku mikono ikiwa juu ya meza kwa mpatanisho wa viganja vyake.
"*Yes,* hata mimi sina shaka naye kabisa, ni askari mwenye uwezo mkubwa, na ujuzi wa kila aina, naamini ataifanikisha hii misheni bila wasiwasi." IGP Edward Kituo aliunga mkono hoja hiyo. Tayari walishauona ugumu wa kitu wanachokitafuta. Bado hawakujua kama ni mtu ama kikundi cha watu, hivyo ikabidi wamtafute mwanaume mmoja muadilifu, mwenye uwezo na kipawa cha hali ya juu apewe kazi hiyo.
DCI Alfred Chigamba akaliweka mezani jina la Azizi Kasese, askari shupavu mwenye cheo cha Inspekta, aliyebarikiwa uwezo mkubwa wa kiufanisi na mapambano. Macho ya Rais profesa Omar Kifaranga, yakawatazama wote walioitawala meza hiyo kwa mtindo wa *"Tunakubaliana?"*. Kwa kutumia sura zao kila mmoja alisadiki, kazi ikawa kwa maafande hao kulitupa jukumu hilo kwa mwanaume waliyemuamini. Mjadala ukafungwa, IGP Edward Kituo akalivalia njuga swala hilo, akawa safu ya mbele kulihudumu. Bila kuchelewa Inspekta Azizi Kasese akatafutwa, ni mtu anaeijua vizuri kazi yake sio masihala.

Muda mchache baaadae, ndani ya ofisi za Makao Makuu ya polisi, Inspekta Kasese akiwa wima mbele ya meza iliyowatenganisha yeye na IGP Edward Kituo, makabidhiano ya majukumu yakafanyika. Akapewa siku tisa pekee, kazi inatakiwa iwe imefikia tamati kwa jibu zuri litakaloyarudisha matabasamu yao upya, kama awali.

* *

Kelele za mdundo mkubwa wa muziki zilizama masikioni mwa waliousikiliza, samani nyingi ghari, na fahari zilitapakaa ndani ya jumba hilo. Thamani zake ziliendana na hadhi ya kasri hilo kubwa na la gharama. Bwawa la kuogelea, magari ya starehe, na vingi vya kuvutia vilionekana. Ilikuwa ndani ya jumba la mtoto wa mzee Kimati Sesewa, tajiri wa juu kabisa kwenye taifa la Takaseni. Muziki ulirindima, vijana wenye mionekano na mitindo ya kisasa walisheheni wakifurahia..
"*Kilichomponza fala, kujiona Simba kumbe swala. Kazama kwenye penzi uchwara, badala kusaka miamala, Aiyooo oo.*


*Toka n'deti Pesa, sasa napendeza. Na tena nainjoi, na wanangu ma'home boy, Oooooh akaunti inasoma, na kamwili kananona, we mwenyewe si unaona. Nasema booora, bora niinjoy, tritititititi."*

Yalikuwa mashairi ya wimbo uliokuwa ukiwaburudisha vijana hao, yaliwapa midadi, hakuna aliyekaa, baadhi walipanda juu ya meza wakirukaruka, ni wazimu mfululizo hadi mwandishi pia kichwa kinasebeneka. Acheni tu. Kwenye eneo la bwawa la kuogelea, wasichana na wavulana wengi walikuwamo wakiiendeleza furaha yao, bila shaka ilikuwa tafrija, ila haikuwa na utambulisho maalum.

"*Babe,* kwahiyo kwa kuendelea kufanya hivi unahisi machungu ya kuwapoteza rafiki zako yatakwisha." sauti ya kike ililitupa swali hilo kwa aliyekuwa akimuuliza.
"Kama hakuna mlango wowote wa wao kurudi tena kwenye ulimwengu huu, basi na mimi sipaswi kuhuzunika milele. Ila sitaacha kuwaombea" alijibu mwanaume, akifunga kauli yake kwa kugida unywaji wake alioutua kando ya bwawa hilo la kuogelea, huku kiwiliwili chake kikiwa majini.
"Mmh, sawa." alipiga funda kadhaa za unywaji wake na yeye, kisha akaendelea, "najua wao ndiyo walikuwa kampani yako kubwa, sasa hawako tena, lazima tu utahisi unyonge mpenzi wangu."
"Kwa sasa sihisi chochote."

"Sawa, ila una mpango wa kufanya nini muda huu ambao uko mwenyewe."
"Niko na wewe Vivi, na nimebakiza jambo moja kubwa la kufanya nikiwa kama mpenzi wako."

**Tukutane toleo lijalo...**



# HADITHI

## "SHEMEJI USIZIME TAA...! NAOGOPA UKIMWI...! - 04

Na. Charles Gululla

**Niliendesha gari taratibu, huku tukiongea na Ray na kutaniana, nikaamua tupitia kwanza Bahama Mama ili kupata vinywaji, kabla ya kuendeleaa na safari yetu. Rehema hakuwa mnywaji, ila alikuwa akilambalamba na alikunywa pombe laini, ambazo mi ninaweza kukesha nikizinywa na nisilewe.**

***Endelea...***

"Lakini Don K kwanini hujaoa mpaka sasa?"
"Sijapata ruhusa ya kuoa kwa wazazi"
"Ati unasemaje!" alishangaa na kunikazia macho, nikarudia jibu langu.
"Ndiyo, sijapata ruhusa toka kwa wazazi. Kwa mila zetu, wazazi ndiyo wenye jukumu la kunioza. Lakini ninaamini, nikikupeleka na kukutambulisha watanioza mara moja"
"Miye bado nasoma Don, mbona una mcheche"
"Acha utani Ray. Aliyeanzisha 'Topic' ya kuoa ni wewe, anyway, niseme hivi, sijaoa kwa sababu nilikuwa nakusubiri wewe" niliongea akabakia akiniangalia tu. Tulipomaliza vinywaji, tuliendelea na safari yetu kuelekea nyumbani kwangu. Tulipofika, niliingiza gari kwenye kasri yangu na kuiegesha pembeni ya ki-HIACE.
"Kweli huku ndio kwako, naona ki-HIACE nacho kimepoa, aisee huku ni kuzuri kweli." Ray alisema na tukashuka, nikamkaribisha ndani. Aliangalia saa yake na kujenga hoja ya kutokukaa sana.
"Sintokaa sana, inabidi unirudishe kwetu mapema sana, nisije kumuudhi mjomba na shangazi"
"Pamoja na binamu yako Hilda" nilisema na nikacheka, kwani nilijua hiyo ndiyo janja ya mabinti wote kujifanya wana haraka na hawataki… kumbe wanataka sana. Nilipomtajia Hilda alicheka na kuninong'oneza, kuwa yeye na Hilda damu damu ndiyo maana mambo yake alimweleza Hilda na hakumweleza mtu mwingine.
"Poa, basi shemeji Hilda ndiyo wetu, msiri wetu na mshirika wetu au vipi" nilisema huku nikimkumbatia Hilda na umbo lake.

Nilimshika mkono, tukaingia ndani. Nikamkaribisha aketi kwenye kiti, name nikaketi karibu naye, mkono wangu ukiwa begani kwake.
"Mimi nilijua leo wewe ni mgeni wangu, utalala hukuhuku, kumbe… Ah! Wataka kuondoka uniache peke yangu, nishaanza kunenepa kuwa pamoja nawe, unataka nikonde," nilimchombeza kwa sauti laini ya kilevilevi.
"Hapana dear, ni mapema mno, mimi kuanza kulala huku kwako. Usiwe na papara" alijitetea.
"Okay, upendavyo wewe, hebu nambie, wapenda kunywa nini darling?"
"Oh my dear, kunywa tena, hapana!"
"Kwa nini, si utaonja kidogo kidogo"
"Hapana dear, inatosha, nisije kupatwa na wazimu"
"Okay, je wapenda kusikiliza nyimbo gani ikuburudishe" nilizungumza huku nikiuzungusha mkono wangu kiunoni  mwake.
"The boy is mine…" alinong'ona kwa upole name nikaruka na kumbusu kwa furaha.
"Umepata dear, sema lingine" nilisema huku kwenda kupachika CD yenye wimbo huo, kisha nikarejea na kuketi sambamba naye.

Kwa jinsi nilivyokuwa na moto naye, nilimkumbatia na kumbusu hapa na pale. Ray alionekana kutopenda, au labda alinionea aibu, nikaamua nimwingize kitaalamu kwenye fani mpaka afurahi mwenyewe. Niliishika shingo yake nikawa naisugua kimahaba. Mokono wangu ukawa ukshuka na kupanda kwenye mgongo wake, kama yule mchezaji nyota wa Real Madrid Mbrazil Roberto Carlos. Kichwa chake nilikilaza magotini pangu, mkono wangu nikauingiza kwenye blauzi yake kuzisaka "Embe Dodo". Nikaipata mojawapo na kuibinya, akashtuka na kusonya. Nikaipikicha kitaalamu, akasisimka na kufumba macho kisha akakunja miguu yake na kujigeuza. Sehemu kubwa ya "maungo" yake (maradhi yangu) yalibakia wazi na wazimu ukanipanda. Nikahamishia mikono yangu juu kidogo ya magoti yake, nikawa navivuta vinyweleo kwenye "maungo" yake. Akagugumia na kuzungumza maneno yasiyoeleweka kwa sauti ya chini. Niliendelea kuyasugua maungo yake huku nikipanda kuelekea kwenye "ngome" ya malkia na nikajipinda kiaina, kwa kasi kubwa nikautumbukiza ulimi kinywani mwake na kuanza kula denda. Uzalendo ukamshinda akaanza kurukaruka. Nikaongeza utundu kidogo kuibugia kinywani mwangu moja ya "embe dodo" zake. Joto lake

na mjazo wake kinywani mwangu ilikuwa ni starehe mwanana. Akalalamika binti wa watu na kutoa mguno, na nilipomtazama machoni, alitoa machozi.

Yalikuwa machozi ya furaha! Nikajua darasa langu limeeleweka na hapo ndipo nilipopataka. Nikaendeleza "utaalamu" wangu na kilio kilipozidi nilitulia kidogo. Akahema mhemo wa mahaba, nikacheka moyoni.
"Aaah D.K siyo leo dear… niache!" alikuwa keshachelewa, kwani wakati huo nilikuwa namalizia kummenya "viwalo" vyake na nikambeba na kumpeleka "graundini".
"Aisee Don una fujo sana. Sikutarajia kama utaniendesha kiasi hiki, umenikongoroa na kuniacha hoi. Yaani wewe! … wewe ni dereva mzuri siyo kwenye gari tu, hata kwenye hii fani umekuwa mwalimu wangu. Ray alilalamika na kuongea baada ya kufikia tamati ya "mechi"yetu ambayo ilinifanya nielewe kwanini watu uhonga mapesa "lukuki". Au kwanini watu huamua kuoa. Kama jamaa yangu fulani alioa akiwa na miaka ishirini tu. Kumbe kisa ni "mahanjamu" yalimkolea, akaamua kubeba "kifaa" awe nacho wakati wote.
Rehema alikuwa kinda sana katika fani kwani nilikiri kuwa mwalimu wake na hakuwa mtaalmu sana, huende mimi nilikuwa mtu wa awali (may be) naweka msisitizo! Kumfanyia vurugu kwenye "himaya" yake na hilo ndilo lililonifanya "nimzimie ile kishenzi".
Nilitaka kumrudisha tena graundini, lakini akaruka na kunikaripia kwa ukali.
"Don! Aah, unataka kunikomoa." Nikasema moyoni kuwa aliyataka mambo mwenyewe wacha yamkute. Lakini nilipomuona anapioga miayo kichovu nilimpa pole na kumbusu.
"Pole sana Ray my dear, yote hiyo ni shauri ya kukupenda and I want to confirm that"
"I know, usijali, ninakupenda pia na nina haki ya kukusifu kuwa u dereva mzuri, umenifikisha nisikokutarajia."
"Thank you dear, nitahakikisha unakuwa wangu kwa gharama yoyote" nilitamba.
"Are you serious" alinihojim nikamjibu ndivyo. Baada ya shughuli nzito ya kulijenga taifa, nilimrudisha Ray Mabibo. Tulipofika tu, Hilda aliyekuwa bado yuko salon alitoka na kuja kwenye gari.
"Afadhali umemrudisha, nilikuwa na wasiwasi…"

***Itaendelea toleo lijalo...***

**ANDIKO NYETI**

**VIRGINIA HALL - MWANAMKE ASIYE NA UMUHIMU — 03**

**Mtandao wa Hall ulijumuisha watu 1,500, akiwemo askari aliyechanganya uraia Mwamerika-Mfaransa ambaye baadae alikuja kuwa mumewe, Paul Goillot. Mpwawe Hall, Lorna Catling, ambaye ana miaka 89 (wakati kikiandikwa kitabu hiki) anayeishi Baltimore, aliomba kukutana na mama yake mkubwa mara baada ya vita.**

"Alikuja nyumbani nilipokuwa na miaka 16, alikuwa amepauka na nywele nyeupe na nguo kama mwendawazimu," Catling anasema.
Na ni kipi Hall alisema kuhusu vita?
"Kamwe hakuzungumza kuhusu hilo," Catling aliongeza.
Uingereza na Ufaransa, zote zinautambua mchango wa Hall – kwa siri. Rais Harry Truman alitaka kumpa Hall heshima hadharani wakati wa sherehe pale White House. Hall alikataa, akasema anataka kubakia undercover (asiyejulikana).
William Donovan, chifu wa OSS, alimpatia nishani ya huduma maalum – alimfanya kuwa mwanamke raia wa kwanza kuipokea katika Vita ya Pili ya Dunia. Mama yake Hall alikuwa mtu pekee kutoka nje White House kuhudhuria sherehe hiyo.
Na Mwandishi wetu
Wakati Vita ya Pili ya Dunia ilipolipuka na kundi la NAZI la Ujerumani kuivamia Ufaransa, mwanamama Hall alijitolea kuendesha gari la wagonjwa la Wafaransa. Haukupita muda, Wafaransa wakamlazimisha kukimbilia Uingereza. Ilikuwa nafasi ya kukutana na ujasusi, hivyo wakamuunganisha na wanaintelijensia wa Kiingereza.
Baada ya mafunzo kidogo, huyu mwanamke Mmarekani mwenye mguu moja alikuwa miongoni mwa majasusi wa kwanza wa Uingereza kutumwa ndani ya NAZI iliyojikita huko Ufaransa mwaka 1941. Akajifanya mwanahabari wa gazeti la New York Post.

Kufuatiliwa na Gestapo
Kulikuwa na makosa, hasa katika siku za mwanzoni, wakati wenzake wa mtandao wake walipokamatwa na kuuawa.
Wajerumani wakagundua kwamba wapo mikononi mwa mwanamke mlemavu.
Lakini Hall alikuwa Jasusi wa kawaida, aliyepiga hatua moja mbele zaidi ya polisi wa siri wa Kijerumani, Gestapo.
"Virginia Hall, kwa upande fulani, alikuwa asiyependa," anasema Gralley. "Aliweza kuwachezea Gestapo anavyotaka. Hakuna hata mmoja wa Wajerumani katika vita ile aliyefikiri kuwa mwanamke huyo anaweza kuwa jasusi."
***Mwendelezo utaukuta toleo lijalo….***

## Tangazo




Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com